JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

**TOLEO MAALUM**

**JUNI 2023**




Air Tanzania Carg
The Wings of Kilimanjaro




Ndege mpya ya Mizigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania ATCL mara baada ya kutua katika uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 03 Juni, 2023

## BODI YA WAHARIRI:

**Mwenyekiti**
Segolena Francis / Christopher Philemon

**Wajumbe**
Shukuru Senkondo
Biseko Ibrahim
Deniza Cyprian
Siti Said

**Msanifu**
Bolgas Odilo

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi
S.L.P 2888 Ujenzi/S.L.P 638 Uchukuzi
**Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.**

Simu: +255 26 23244455
Barua pepe: ps@mow.go.tz

Tufuatilie katika kurasa zetu kwenye mitandao ya kijamii

wizarayaujenzinauchukuzi www.mwt.go.tz

# HAFLA YA MAPOKEZI YA NDEGE MPYA YA MIZIGO AINA YA BOEING 767-300F NA RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Na **Jacob Kipara**




*Ndege mpya ya Mizigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania ATCL ikiwasili na kumwagiwa maji "watersalute" mara baada ya kutua katika uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 03 Juni, 2023.*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa na Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango, Rais wa Zanzibar Mhe. Hussein Ali Mwinyi, Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa pamoja na viongozi wengine wakati akikata utepe kuzindua Ndege mpya ya Mizigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania ATCL kwenye hafla fupi iliyofanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 03 Juni, 2023.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa amekaa kwenye Chumba cha Marubani ya Ndege mpya ya Mizigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania ATCL mara baada ya kuizindua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 03 Juni, 2023.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na Marubani walioileta Ndege mpya ya Mizigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania ATCL*

# DKT. MPANGO AWEKA JIWE LA MSINGI BARABARA YA MIANZINI - NGARAMTONI JUU KM 18

Na **Segolena Francis**




*Makamu wa Rais Dakta, Philip Mpango akisisitiza jambo kwa wananchi hawapo pichani wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara ya Mianzini-Ngaramtoni juu KM 18 wilayani Arumeru mkoani Arusha.*

Makamu wa Rais Dakta, Philip Isdor Mpango amezungumzia umuhimu wa wananchi kutumia kwa usahii barabara zinazojengwa kwa kiwango cha lami ili kuepuka ajali na kuzilinda barabara hizo kwa kutunza mazingira.

Akizungumza wakati akiweka jiwe la msingi barabara ya Mianzini-Ngaramtoni juu KM 18 inayojengwa kwa kiwango cha lami jijini Arusha Dakta, Mpango amesema ni vema jamii ikatambua kuwa barabara zinajengwa kwa fedha nyingi za wananchi hivyo wanalazimika kuzilinda na kuzitunza ili zidumu na kuleta tija kwa wananchi.

"Tunajenga barabara za lami kila mahali hivyo nitoe wito kwa watumiaji wa barabara kuwa makini na kuendesha vyombo vya moto kwa tahadhari ili kuepuka ajali, ulemavu na vifo na wananchi kuacha shughuli za binadamu zinazofanyika kwenye njia za maji kwani husababisha mafuriko wakati wa mvua na kuharibu barabara", amesisitiza Makamu wa Rais Dakta, Mpango.

Aidha amemtaka mkandarasi anayejenga barabara hiyo kutoa kipaumbele cha ajira wa vijana wa mkoa wa Arusha ili waweze kunufaika kiuchumi na kitaalam na hivyo kuulinda mradi huo.




*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akifafanua jambo wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara ya Mianzini-Ngaramtoni juu KM 18 wilayani Arumeru mkoani Arusha.*

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amesema barabara Mianzini-Ngaramtoni juu KM 18 ikikamilika licha ya kupunguza msongamano katikati ya jiji la Arusha pia itawezesha wafanyabiashara na watalii kufikia masoko na vivutio vya utalii kwa urahisi.

"Ujenzi wa barabara hii unalenga kuzifungua barabara za Wilaya ya Arumeru kwa kupita katika maeneo ya uzalishaji na hivyo kukwepa msongamano katikati ya jiji la Arusha", amesisitiza.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS Eng. Rogatus Mativila amesema ujenzi wa barabara ya Mianzini-Ngaramtoni juu KM 18 umegawanywa katika sehemu tano ili kurahisisha kazi ya ujenzi na utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 22 utakapokamilika.




*Makamu wa Rais Dakta, Philip Mpango akisalimiana na Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya (wapili kulia), na viongozi wengine alipokwenda kuweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara ya Mianzini-Ngaramtoni juu KM 18 wilayani Arumeru mkoani Arusha.*



*Mtendaji Mkuu wa TANROADS Eng. Rogatus Mativila akifafanua jambo kwa Makamu wa Rais Dakta, Philip Mpango wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa barabara ya Mianzini-Ngaramtoni juu KM 18 wilayani Arumeru mkoani Arusha.*

# MAZINGIRA YA BIASHARA NCHINI YAVUTIA SHIRIKA LA NDEGE LA SAUDIA

Na **Christopher Philemon**




*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa akiwa na Kaimu Balozi wa Saudi Arabia Nchini, Mhe. Fahad Alharbi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk na viongozi mbalimbali wa Sekta ya Uchukuzi akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa safari za ndege za Shirika la Saudia katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere kutokea Nchini Saudia Arabia, jijini Dar es Salaam.*

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu itahakikisha mazingira ya biashara ya ndani na nje yanaimarishwa ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi kufanya biashara na Tanzania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mara baada kupokea ndege ya kwanza aina ya Airbus A320 ya Shirika la Ndege la Saudia iliyotua kwa safari yake ya kwanza nchini kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Waziri Prof. Mbarawa amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha viwanja vya ndege nchini vinatumiwa na mashirika mengi zaidi ili kuinua pato na kukuza biashara na utalii.

"Niwahakikishie ndugu wananchi kuwa Serikali imeamua kuifungua nchi kupitia anga lake, na kama mnavyoona mashirika ya ndege yanaendelea kuja nchini kupitia katika viwanja vyetu hii ni dalili nzuri katika kukuza pato na kuimarisha biashara kati yetu na nchi nyingine" amesema Waziri Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa amesema usafiri wa anga umeendelea kukua siku hadi siku kwani kumekuwa na ongezeko la idadi ya abiria katika kiwanja hicho kutoka abiria milioni Moja na Laki Sita kwa mwaka 2021 hadi abiria milioni Milioni Mbili na Laki Sita kwa mwaka 2023 ongezeko ambalo limeifungua Tanzania kibiashara na kiuchumi.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk amesema Tanzania na Saudia Arabia zimekuwa zikifanya biashara ya nyama na mboga mboga hivyo uwepo wa safari za ndege za shirika hilo utarahisisha usafirishaji na kukuza biashara baina ya nchi hizo mbili.

Naye Kaimu Balozi wa Saudi Arabia Nchini, Mhe. Fahad Alharbi amesema Tanzania na Saudia Arabia zimekuwa na mashirikiano katika Nyanja mbalimbali hivyo kupitia usafiri wa anga mahusiano yataboreshwa zaidi kwani abiria

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu itahakikisha mazingira ya biashara ya ndani na nje yanaimarishwa ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi kufanya biashara na Tanzania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mara baada kupokea ndege ya kwanza aina ya Airbus A320 ya Shirika la Ndege la Saudia iliyotua kwa safari yake ya kwanza nchini kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Waziri Prof. Mbarawa amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha viwanja vya ndege nchini vinatumiwa na mashirika mengi zaidi ili kuinua pato na kukuza biashara na utalii.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) Mussa Mbura akizunngumza na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuhusu utendaji wa Viwanja vya ndege nchini, wakati wa hafla wa mapokezi ya ndege ya Shirika la Saudia iliyotua kwa mara ya kwanza katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA) kutokea Nchini Saudia Arabia, jijini Dar es Salaam.*



*Kaimu Balozi wa Saudi Arabia Nchini, Mhe. Fahad Alharbi (kushoto) akizungumza na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (wa pili kulia) na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Katikati) hafla wa mapokezi ya ndege ya Shirika la Saudia iliyotua kwa mara ya kwanza katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere kutokea Nchini Saudia Arabia, jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk wakizungumza katika hafla wa mapokezi ya ndege ya Shirika la Saudia iliyotua kwa mara ya kwanza katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA) kutokea Nchini Saudia Arabia, jijini Dar es Salaam.*



# DKT. MPANGO AAGIZA UJENZI ZAIDI BARABARA ZA LOLIONDO

Na **Shukuru Senkondo**



*Muonekano wa barabara ya Mto wa Mbu - Loliondo sehemu ya Waso –Sale KM 49 wilayani Ngorongoro mkoani Arusha.*

Makamu wa Rais Dakta, Philip Isdor Mpango ameitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuanza kujenga sehemu ya tatu ya barabara ya Mto wa Mbu hadi Loliondo KM 217, (sehemu ya Ngaresero - Engaruka KM 39.2) ili kurahisisha huduma za usafiri, uchukuzi na utalii wilayani Ngorongoro.

Akizungumza wakati akifungua rasmi barabara ya Mto wa Mbu - Loliondo sehemu ya Waso –Sale KM 49 , Dakta, Mpango amesema nia ya Serikali ni kuijenga na kuikamilisha barabara yote lakini kwa hatua ya sasa ni vema ikajengwa sehemu ya tatu mara baada ya kukamilika kwa sehemu ya kwanza.

"Najua kuwa mmeshaisanifu barabara yote toka Mto wa Mbu hadi Loliondo KM 217, sasa baada ya kumaliza sehemu ya kwanza ya Waso-Sale KM 49, hamieni sehemu ya tatu ya Ngaresero - Engaruka KM 39.2 kwa kuwa sehemu hiyo ina changamoto nyingi kwa wasafiri na wasafirishaji", amesema Dakta, Mpango.

Ameitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuhakikisha barabara kuu na za mikoa zinapitika wakati wote wa mwaka na kuwataka wananchi kuzitunza na kuzilinda ili zidumu kwa muda mrefu na kuleta tija kwa wafugaji, wakulima, wafanyabiashara na watalii na hivyo kuchochea maendeleo.

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amesema Wizara itaendelea kuhakikisha inafanya matengenezo maalum ili sehemu ya pili ya Sale-Ngaresero KM 57.4 na sehemu ya nne ya Engaruka- Mto wa Mbu KM 60.9 nazo ziwe katika ubora na kupitika wakati wote wa mwaka.

Aidha amesema Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), umepanga kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Waso-Loliondo KM 10 ili kuunganisha na kuupendezesha mji wa Loliondo.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS Eng. Rogatus Mativila amesema barabara ya Waso –Sale KM 49 imejengwa na mkandarasi China Wu Yi Co. Ltd kwa zaidi ya shilingi bilioni 87 na kukamilika kwake kutachochea ustawi wa sekta nyingine za kiuchumi hususan utalii,kilimo na ufugaji.

# KARAKANA YA VICHWA VYA TRENI TRC YATAKIWA KUWEKEZA KATIKA KUZALISHA WATAALAM NA VIFAA

Na **Juhudi Mmari**



*Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi anayeshughulikia Sekta ya Uchukuzi Mhe Atupele Mwakibete akifafanua jambo kwa Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mhe Selemani Kakoso na Wajumbe wa kamati hiyo wakati wakitembelea na kukagua Karakana ya Ukarabati wa Vichwa vya Treni ya kawaida-MGR Mkoani Morogoro.*

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya miundombinu Mhe Seleman Kakoso ameitaka TRC Kuwekeza kwenye Karakana ili iweze kuzalisha wataalamu na vifaa ambavyo kwa sasa vinaletwa kutoka nchi za nje kwa ajili ya ujenzi,ukarabati na utekelezaji wa miradi ya Reli Nchini

Ameyasema hayo leo wakati kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilipotembelea na kukagua karakana ya ukarabati wa vichwa vya Treni ya kawaida-MGR iliyopo Mkoani Morogoro

"Wekeni bajeti nzuri ambayo itasaidia karakana kutengeneza vifaa ambavyo vinawezekana kutengenezwa hapa Nchini, ukizingatia tunaelekea kipindi cha bajeti kuu ya Serikali hivyo shirikianeni na Wizara na sisi kama kamati tupo tayari kuwaunga mkono" amesisitiza Mhe Kakoso

Kwa upande wake Naibu Waziri Sekta ya Uchukuzi, Mhe Atupele Mwakibete amesema Serikali ya Awamu ya sita inaeendelea kutenga Fedha kwa ajili ya kukarabati vichwa na mabehewa ya treni ili kuboresha huduma ya Reli ya kati Nchini ambapo tarehe 30 juni, 2021 Serikali ya awamu ya sita iliiingia mkataba wa Dola za Kimarekani Mil 10.5 na kampuni ya SMH RAIL kutokea nchini Malaysia kwa kutumia karakana ya Morogoro kufanya ukarabati mkubwa wa vichwa vya treni ya kawaida-MGR.

"Ukarabati huu ni wa kufufua vichwa vya treni ya kawaida tisa vya Reli ya kati ambapo viwili ni vya njia kuu na saba ni vya sogeza na unaohusisha ufungaji wa vipuri vipya, Engine Mpya, Bogi mpya na unatarajiwa kukamilika ifikapo julai,2023." amesisitiza Mhe Mwakibete

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la reli Tanzania bi Amina Lumuli amesema Karakana ya Vichwa vya

Treni Morogoro inakumbana na changamoto mbalimbali kama vile ugumu wa upatikanaji vipuri kwa wakati, pamoja na upungufu wa rasilimali fedha.

Shirika la Reli Tanzania lina jumla ya vichwa vya Treni ya kawaida-MGR 59,vichwa 43 vikiwa vya njia kuu na 16 vikiwa vya Sogeza na kati yake vichwa vinavyofanya kazi ni 44 ambapo vichwa 30 ni njia kuu na vichwa 14 sogeza na limeendelea kukuza wataalamu wa ndani kwa kuwapatia ujuzi wa kimasomo ndani na nje ya nchi ili kuendana na teknolojia ya kisasa na mabadiliko ya mara kwa mara ya vipuri kwa minajili ya kuboresha usafiri wa reli ya kawaida Nchini kwa maslahi ya Taifa.




*Kichwa cha Treni ya kawaida-MGR cha kuvutia mabehewa ya abiria na mizigo kwa njia kuu aina ya 88 class kikifanyiwa ukarabati ndani ya Karakana ya Ukarabati wa Vichwa vya Treni ya kawaida-MGR Mkoani Morogoro*

# UKAGUZI



*Naibu Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi, Dkt. Ally Possi akikagua utoaji wa huduma katika  Bandari ya Mtwara.*

# DKT. MPANGO ATAKA BARABARA YA KABINGO - KASULU - MANYOVU KUKAMILIKA KWA WAKATI

Na **Segolena Francis**



*Muonekano wa barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu yenye urefu wa kilometa 260.6 ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami unaendelea mkoani Kigoma.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango ameitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuhakikisha ujenzi wa barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu yenye urefu wa kilometa 260.6 unakamilika kwa wakati na ufanisi uliokusudiiwa.

Amesema hayo Wilayani Kasulu alipokutana na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) na viongozi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na kusisitiza kuwa kukamilika kwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ndio utakuwa ukombozi wa uchumi wa mkoa wa Kigoma na kanda ya magharibi kwa ujumla.

“Wananchi wengi wa Kasulu, Kibondo na Kakonko wanafanya biashara nyingi Kahama, Shinyanga na Mwanza hivyo kukamilika kwa barabara hii kutakuza uchumi wa wakazi wengi wa mkoa wa Kigoma”, amesema Dkt. Mpango.

Amesisitiza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), kuongeza kasi ili kukidhi matarajio ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuufungua Mkoa wa Kigoma katika Nyanja zote za usafiri.

Naye Mwenyekiti wa PIC Mhe. Jerry Silaa amemweleza Makamu wa Rais kuwa Kamati yake imekagua uwekezaji wa Serikali mkoani Kigoma na imeridhika kwa kazi nzuri zinazofanywa katika usafiri wa reli, bandari, barabara na anga na kumhakikishia Makamu wa Rais kuwa kamati hiyo itakagua miradi hiyo mara kwa mara ili kuhakikisha uwekezaji unaofanywa unakuwa na tija kwa wananchi.

“TANROADS hakikisheni ujenzi wa barabara licha ya kutoa fursa kwa wananchi bali uwezeshe wakandarasi wetu kupata ujuzi na hivyo kumudu kujenga na kusimamia miradi mikubwa siku za usoni”, amesesitiza Mhe. Silaa.

Aidha, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (sekta ya ujenzi), Bw, Ludovick Nduhiye amesema Wizara imejipanga kuhakikisha mkoa wa Kigoma unafikika kwa urahisi kupitia barabara zake zote, reli, bandari na anga ili kuuunganisha na masoko ya nchi za Congo, na Burundi kwa urahisi na hivyo kukuza shughuli za kilimo, biashara na uwekezaji.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS Eng. Rogatus Mativila amesema barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu yenye urefu wa kilometa 260.6 ni sehemu ya barabara kuu ya Nyakanazi-Kibondo-Kasulu-Manyovu inayounganisha mkoa wa Kigoma na mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga na Mwanza na pia inaunganisha Tanzania na Burundi kupitia mpaka wa Manyovu.

barabara ya kikanda yenye lengo la kuufungua ukanda wa magharibi na kuiunganisha Tanzania na Burundi.
Eng. Mativila amesema katika kuhakikisha ujenzi wa barabara hiyo ya kikanda unakwenda kwa haraka mradi umegawanywa katika sehemu nne ambapo zaidi ya shilingi bilioni 325.6 zinatarajiwa kutumika katika kuwalipa wakandarasi wanne wanaojenga barabara hiyo wakati takriban shilingi bilioni 15.37 zikitengwa kuwalipa wasimamizi wake.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), iko mkoani Kigoma kukagua utekelezaji wa miradi ya Serikali ambapo pamoja na mambo mengine imekagua, imeelekeza na kuelezea kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa barabara hiyo ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami unatarajiwa kukamilika baadae mwaka huu.



*Aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila akifafanua jambo kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango alipokagua barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu yenye urefu wa kilometa 260.6 Mkoani Kigoma.*

# HISTORIA MPYA MIUNDOMBINU YA KIMKAKATI KUANDIKWA

Na **Christopher Philemon**



**PICHANI:** *Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa, akijibu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na waheshimimwa wabunge waliochangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bungeni Jijini Dodoma.*

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kauli moja limeridhia na kuidhinisha zaidi ya shilingi trilioni 3.5 kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Bajeti hiyo pamoja na mambo mengine inatarajiwa kuweka historia nchini ambapo barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa kilometa 2,035 zinatarajiwa kujengwa kwa kiwango cha Lami na kuchochea ukuaji wa uchumi katika maeneo mbalimbali.

Akijibu hoja za wabunge wakati wa majumuisho ya bajeti ya Wizara hiyo Bungeni jijini Dodoma Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kwa dhati kuifungua nchi kiuchumi kupitia miundombinu ya kimkakati inayosimamiwa na Wizara kwa upande wa Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi.

Prof. Mbarawa amezitaja barabara 7 zenye urefu wa kilometa 2,035 zitakazojengwa kwa utaratibu wa EPC + F kuwa ni barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha/ Songea (km 435), barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (Simiyu) (km 339) na barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboroti – Mrijochini – Dalai – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460).

Miradi mingine ni barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa Junction (km 453.42), barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale (km 175), barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218), barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe yenye urefu wa kilometa 48.9 pamoja na barabara ya Mafinga – Mtwango – Mgololo (km 81).

Aidha, barabara ya Express way kutoka Kibaha-Chalinze-Morogoro ambayo ujenzi wake unashirikisha

sekta binafsi itajengwa huku miradi ya mabasi ya mwendo kasi ya DART na daraja la Jangwani vikitengewa Bilioni 2.2.`

Kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi shilingi Trilioni 1.13 zinatarajiwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), ikiwemo vipande vipya vya Dodoma hadi Kigoma, Uvinza hadi Burundi na DRC.

Ununuzi na utengenezaji wa ndege nne utakaogharimu takriban shilingi bilioni 300 utatekelezwa ukiwa ni mkakati wa kuendelea kuifufua ATCL ili kulifanya shirika hilo kuwa na tija na kuchagiza uchumi nchini.

Profesa Mbarawa amesema Serikali imejipanga kuhakikisha huduma za usafiri wa anga, utabiri wa hali ya hewa na usafiri kwa njia ya maji zinakuwa salama na za uhakika.

Jumla ya wabunge 75 wamechangia katika bajeti hiyo ambapo kati ya hao 67 kwa kuongea na nane kwa maandishi. Na hatimaye bunge kupitisha kifungu kwa kifungu Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.



*Naibu Waziri wa Ujenzi Mha. Godfrey Kasekenya, akijibu hoja za wabunge wakati Bunge likipitisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24, Bungeni Jijini Dodoma*





*Naibu Waziri wa Uchukuzi Atupele Mwakibete, akijibu hoja za wabunge wakati Bunge likipitisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24, Bungeni Jijini Dodoma.*

# RUFIJI WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA

Na **Deniza Cyprian**




**PICHANI:** *Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya, akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Rufiji (hawapo pichani) mara baada ya kuweka saini mikataba wa ujenzi wa barabara ya Nyamwage hadi Utete (km 33.7) kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Daraja la Mbambe (m 81) na barabara unganishi (Km 3), wilayani humo mkoani Pwani.*

Wananchi wa Wilaya ya Rufiji mkoa wa Pwani wametakiwa kutumia fursa ya ujenzi wa barabara za lami ili kukuza biashara.

Wito huo umetolewa na Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya mara baada ya kushuhudia utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Nyamwage hadi Utete (km 33.7) kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi wa Daraja la Mbambe (m 81) na barabara unganishi (Km 3) kati ya Wakala wa Brabara (TANROADS), na kampuni za China Railway Seventh Group na Nyanza Road Works ya Tanzania.

"Ujenzi wa barabara hii na daraja utafungia fursa za usafirishaji wa abiria, mizigo, mazao ya biashara, misitu na kuvuta watalii hivyo hii iwe chachu kwa wakazi kufungua biashara mbalimbali zitakazoinua uchumi wa Wilaya hii", amesema Eng. Kasekenya.

Amesema ujenzi huu ni mkakati na miapango ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuboresha miundombinj ya barabara na madaraja nchini ili kuondoa kero kwa wananchi na kuunganisha barabara za mikoa na wilaya ya nchi nzima.

Aidha, ameongeza kuwa ujenzi wa barabara pamoja na daraja hilo utatumia fedha za ndani kwa asilimia mia moja hivyo jukumu la kulinda vifaa vya ujenzi na kuvitunza ni la kila wananchi ili viweze kuleta matokeo chanya kwa Wilaya.

Ametoa agizo kwa TANROADS kuhakikisha anawasimamia wakandarasi hao ikiwezekana mradi ukamilike kabla ya wakati na kwa thamani halisi ya fedha.

Kwa upande wake Mbunge wa jimbo la Rufiji ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa takriban bilioni 70 kwa ajili ya mradi huo kwani utaifungua Rufiji na kuifanya kuwa kituo cha maendeleo kwa mkoa wa Pwani.

“Wananchi wameisubiri barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami tangu mwaka 1970 bila mafanikio na kwa ujenzi huu Rais Samia ameingia mioyoni mwa wana Rufiji”, amesema Mchengerwa.

Akitoa taarifa ya mradi Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Eng. Rogatus Mativila ameeleza kuwa ujenzi wa barabara hiyo utajengwa na mkandarasi kutoka Kampuni ya China Railway Seventh Group Co., Ltd. ya nchini China kwa gharama ya Shilingi TZS 43,419,537,043.19, bila kujumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa muda wa Miezi 24 na huku ujenzi wa Daraja la Mbambe utajengwa na Mkandarasi kutoka Kampuni ya Nyanza Road Works Ltd ya Tanzania kwa gharama ya Shilingi 24,164,904,622.00 kwa muda wa miezi 24.

Ameongeza kuwa daraja hilo litakuwa na upana wa mita 10.5 ambapo mita 7.5 zitatumika kwa ajili ya kupita magari na mita 2.5 kwa ajili ya waenda kwa miguu na waendesha baiskeli.

Akitoa salam za Mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi na maboresho ya miundombinu inayoendelea mkoa wa Pwani na kuwahakikishia wakandarasi kuwa mkoa huo uko salama na watakuwa pamoja nao wakishirikiana.




*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya, akiwa na Mbunge wa Rufiji ambaye pia ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, wakishuhudia utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Nyamwage hadi Utete (km 33.7) kwa kiwango cha lami kati ya Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mkandarasi kutoka Kampuni ya China Railway Seventh Group, wilayani Rufiji mkoani Pwani.*



*Muonekano wa sehemu ya barabara Nyamwage hadi Utete (km 33.7) ambayo mkataba wa ujenzi wake kwa kiwango cha lami umesainiwa na kushuhudiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, wilayani Rufiji mkoani Pwani.*

# UJENZI WA BARABARA YA UVINZA - MALAGARASI (KM 51.1) WAFIKIA ASILIMIA 31

Na **Siti Said**



*Muonekano wa hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa barabara Uvinza hadi Malagarasi yenye urefu wa Kilometa 51.1 inayojengwa kwa kiwango cha lami, Mkoani Kigoma.*

Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), imesema ujenzi wa barabara ya Malagarasi-Ilunde-Uvinza yenye urefu wa kilometa 51.1 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 31 ya utekelezaji wake na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2023.

Hayo yamesemwa na Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Ngoko Mirumbe wakati wa Ziara ya Waandishi wa Habari katika miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa mkoani humo.

Mhandisi Mirumbe amesema Serikali imelenga kuhakikisha inaiunganisha mikoa yote nchini kwa barabara za lami jitihada ambazo zinajidhihirisha kwa uwepo wa miradi mingi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ndani ya mkoa wa Kigoma na hivyo kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji ili kuchangia uchumi wa mkoa na Taifa kwa ujumla.

"Ujenzi wa barabara hii ni moja ya uwepo wa miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa kwa kasi ndani ya mkoa ambayo inaashiria kwamba ndani ya muda mchache sana kutoka sasa Mkoa wa Kigoma utakuwa umeshaunganishwa kwa miundombinu ya barabara za kiwango cha lami"amefafanua Mhandisi Mirumbe

Amesema kuwa mradi wa Malagarasi-Ilunde-Uvinza ni sehemu ya barabara kutoka Kigoma-Uvinza-Malagarasi yenye urefu wa kilometa 212 ambapo kati ya hiyo kilometa 105 kutoka Kigoma hadi Uvinza zikiwa zimeshajengwa kwa kiwango lami tayari na sasa hadi kuelekea Tabora zimesalia Kilometa 61 ambazo zote mkandarasi yuko site akiendelea na kazi.

Amesema ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami unagharimu zaidi ya shilingi bilioni 62 na mradi unatekelezwa kupitia mkandarasi STECOL Cooperation chini ya Mhandisi Mshauri Norplan Tanzania

Aidha amebainisha kuwa mradi umeajiri wafanyakazi 216 kati yao wafanyakazi wageni wakiwa ni 21 pekee.

Naye Kaimu Mhandisi Mkazi, Mhandisi Yusuf Karera amesema, hadi sasa kazi mbalimbali za utekelezaji wa mradi huo zimefanyika ikiwemo kujenga makaravati 22 huku makaravati madogo yakiwa ni 19 na makaravati makubwa matatu.

# MWAKIBETE AWATAKA NIT KUONGEZA KOZI USAFIRI WA ANGA

Na **Biseko Ibrahim**




*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akimkabishi mmoja wa Wajumbe wa Baraza la 12 la Uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) Alphonce Mwingira mara baada ya kuzindua kozi maalum kwa uongozi huo mpya jijini Tanga.*

Serikali imekitaka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kuhakikisha kinakamilisha taratibu za kupata ithibati na kuanza kufundisha kozi ya usafiri wa anga ili kuiwezesha sekta hiyo kuwa na idadi kubwa ya wataalam wanaoendana na ukuaji wa teknolojia nchini.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo maalum kwa Baraza la 12 la Uongozi wa Chuo hicho yanayofanyika mkoani Tanga, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amesema kuanza kwa kozi hizo kutaenda sambamba na kasi ya Serikali inayofanya kwenye ununuzi wa ndege nchini.

"Serikali inaendelea kununua ndege na ikumbukwe kuwa ndege hizi ni mpya hivyo uwepo wa ndege hizi bila kuwa na wataalam wa kutosha na chuo hiki tunacho hatutakuwa tunatenda haki, hivyo mjitahidi mwaka huu kozi zianze", amesema Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete ameeleza umuhimu wa Baraza hilo kuhakikisha maslahi ya watumishi yanazingatiwa ili kutoa motisha kwa uzalishaji wa wataalam wenye weledi na sifa kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

Aidha, Naibu Waziri Mwakibete ameuhakikishia uongozi wa NIT kuwa Serikali itaendelea kuboresha Chuo hicho kwa kukiwezesha kwenye miundombinu ili kiweze kuzalisha wataalam wa kutosha kwenye njia zote za usafirishaji ikiwemo maji, anga na nchi kavu.

Kwa upande wake Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa amemhakikishia Naibu Waziri Mwakibete kuwa Chuo hicho kiko tayari kuzalisha wataalam hao kwani sasa hivi kinaendelea na tafiti mbalimbali za kuhakikisha kinazingatia ubora kwenye uzalishaji wa wataalam.

Prof. Mganilwa amesema tayari kozi maalum imeanza kwa kuzingatia miradi mikubwa inayoendelea nchini ikiwemo wataalam wa reli ya Kisasa ya SGR, wahandisi na wahudumu wa ndege katika ngazi zote.

Naye Mkurugenzi Msaidizi Utawala Hamid Mbegu, amesema Wizara imeendelea kuhakikisha chuo kinapata Baraza kwa wakati ili kutoathiri utendaji wake kwani Baraza hilo lina maamuzi kwa maendeleo ya chuo.

# ERB ONGEZENI IDADI WAHANDISI WASHAURI

Na **Neema Macha**



*Katibu Mkuu Sekta ya Ujenzi Balozi, Eng. Aisha Amour akiwa ameongozana na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) Eng. Adv. Menye Manga (kushoto kwake) pamoja na Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) Eng. Bernard Kavishe (kulia kwake) akiwasili katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere tarehe 9 Juni 2023 kwenye Mkutano wa Mashauriano ya Wahandisi Washauri.*

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour amezungumzia umuhimu wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi nchini, ERB kuwawezesha wahandisi washauri wazawa ili kunufaika na kasi ya ukuaji wa uchumi nchini.

Akifungua, Mkutano wa wataamu wa Wahandisi Washauri jijini Dar es Salaam leo, Balozi Amour amesema ukuaji wa uchumi unaoendelea nchini lazima uendane na ukuaji wa kada ya wahandisi washauri wazawa, na hivyo kuliwezesha Taifa kuwa na wataalamu wengi watakaofanya kazi ndani na nje ya nchi.

"Idadi ya kampuni za wahandisi washauri zaidi ya 230 na wahandisi washauri 300 haitoshi, hivyo ibueni mifumo itakayorahisisha wataalam wengi wa kihandisi kusajiliwa kuwa wahandisi washauri na kuweka madaraja mbalimbali ya kada hiyo ili kuongeza ushindani", amesema Balozi Aisha Amour.

Katibu Mkuu huyo amesema nia ya Serikali ya Awamu ya sita ni kuhakikisha wahandisi wengi zaidi wanatumika katika miradi ya ujenzi na hivyo kunufaika na fedha nyingi zinazolipwa kwa wahandisi washauri kutoka nje ya nchi.

"Punguzeni masharti ya kusajili wahandisi washauri, hamasisheni wahandisi washauri waliopo kuomba kazi katika miradi inayoendelea, ili fedha nyingi inayoendesha miradi hiyo ibaki nchini", amesisitiza Balozi, Eng. Aisha Amour.

Kwa upande wake Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi, ERB, Eng. Bernard Kavishe amesema Bodi imejipanga kuhakikisha maazimio yatakayofikiwa kwenye mkutano huo yanafanyiwa kazi kwa haraka ili kuwawezesha waandisi washauri kuongezeka na kumudu ushindani kaitka soko la ndani na nje ya nchi.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, (Sekta ya Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour amezungumzia umuhimu wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi nchini, ERB kuwawezesha wahandisi washauri wazawa ili kunufaika na kasi ya ukuaji wa uchumi nchini.

Akifungua, Mkutano wa wataamu wa Wahandisi Washauri jijini Dar es Salaam leo, Balozi Amour amesema ukuaji wa uchumi unaoendelea nchini lazima uendane na ukuaji wa kada ya wahandisi washauri wazawa, na hivyo kuliwezesha Taifa kuwa na wataalamu wengi watakaofanya kazi ndani na nje ya nchi.

"Idadi ya kampuni za wahandisi



*Picha ya pamoja ikimuonesha Balozi Eng. Aisha Amour (watatu kutokea kulia, mstari wa mbele) akiwa pamoja na viongozi wa Bodi ya usajili wa wahandisi katika picha ya pamoja na baadhi Wahandisi Washauri waliohudhuria Mkutano wa Mashauriano ya Wahandisi Washauri katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere tarehe 9 Juni 2023*



*Pichani ni Wahandisi Washauri wakifatilia hotuba ya Mgeni Rasmi (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Mashauriano ya Wahandisi Washauri uliofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere tarehe 9 Juni 2023*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
BODI YA MFUKO WA BARABARA
UHURU NA UMOJA
Roads Fund Board
Financing
Monitoring
Management
TOA TAARIFA YA HALI YA BARABARA SASA
Ni Rahisi
1 Fungua "Play Store" au "App Store"
2 Tafuta neno "Barabara"
3 Bonyeza kitufe cha "Install" Mpaka ifike 100%
4 Bonyeza kitufe cha "Open" fuata maelekezo ya kutoa taarifa ya hali ya barabara
PAKUA BARABARA APP
Google Play
App Store
Mfuko Wa Barabara Tanzania
Toa Taarifa
Taarifa
Mawasiliano
Jinsi ya Kutuma
huduma hii ni BURE
rfb_tz
rfbtz
+255262963277/8
www.roadsfund.go.tz

# SERIKALI YAAHIDI KUENDELEA KUIWEZESHA TAZARA

Na **Biseko Ibrahim**



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (kulia) na Mshauri wa Waziri kutoka Ubalozi wa China Nchini, Suo Peng (kushoto) wakiweka maua katika moja ya makaburi ya Wahandisi na watendaji waliofariki katika ujenzi wa reli ya Shirika la reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), jijini Dar es Salaam. Aprili 1, 2023*

Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete amesema Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuwekeza kwenye Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kuhakikisha shirika hilo linapata faida na kuweza kujiendesha.

Akizungumza katika tukio maalum la kuwakumbuka wahandisi na watumishi mbalimbali waliofariki wakati wa ujenzi wa reli hiyo jijini Dar es Salaam Naibu Waziri Mwakibete amesema mchango walioutoa katika ujenzi wa reli unathaminiwa hivyo Serikali itaendelea kuutambua kwa kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa kutimizwa kiutendaji yanafikiwa.

“Reli hii iliasisiwa na viongozi wetu Hayati Mwl. Julius Nyerere na Hayati Dkt. Kenneth Kaunda aliyekuwa Rais wa Zambia kwa kushirikiana na China hivyo njozi yao ya uanzishwaji wa reli hii hatutaiacha iende hivi kwa kuangalia shirika hili likijiendesha kwa hasara wakati wao walihakikisha shirika linakuwepo na linakuwa na malengo ya kusafirisha mzigo na abiria kwa Tanzania na Nchi Jirani zinazotuzunguka’ amesema Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete amesema Serikali za Tanzania na Zambia kwa kushirikiana na Serikali ya China wako katika hatua mbalimbali za kutatua changamoto zilizopo kwa sasa ili kuhakikisha uwekezaji unaowekwa kwa pamoja unakuwa na tija kwenye miundombinu na mtaji.

Naye Mshauri wa Waziri kutoka Ubalozi wa China Nchini, Suo Peng amemuhakikishia Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, kuwa nchi hiyo iko tayari wakati wote kuhakikisha shirika hilo linaboreshwa kwani lilidhamiria kusaidia kwenye ujenzi hivyo hakuna sababu ya kushindwa kulisaidia kwenye kipindi hiki cha maboresho.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA, Mhandisi Bruno Ching’ amesema TAZARA inatekeleza mpango wake wa muda mrefu na mfupi ambapo kwa sasa tayari kuna kampuni ambazo zinashirikiana nazo ili kuhakikisha uwekezaji unaoendelea kuwekwa unakuwa na faida.

# BARABARA ZA KIGAMBONI KUJENGWA KWA LAMI

Na **Neema Macha**



*Naibu Waziri wa Ujenzi Mhandisi Godfrey Kasekenya*

Serikali imesema itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara za wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam kwa kuzijenga kwa kiwango cha lami kama ilivyopangwa.

Akijibu swali Bungeni leo lililoulizwa na Mbunge wa Kigamboni Dakta, Faustine Ndugulile aliyetaka kujua ni lini Serikali itazijenga barabara za Kibada – Mwasonga – Tundwi hadi Songani na ile ya Ngomvi – Kimbiji hadi Pembamnazi kwa kiwango cha lami, Naibu Waziri wa Ujenzi Mhandisi Godfrey Kasekenya amesema zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwi - Songani - Kimbiji yenye urefu wa kilometa 41 zimetangazwa tangu Januari 6 mwaka huu na zinatarajiwa kufunguliwa Februari, 17, 2023.

Kuhusu barabara ya Chimala-Itamba-Makete yenye urefu wa KM 58 Naibu Waziri Kasekenya amesema Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuijenga barabara hiyo kwa lami na hivyo kuchochea utalii katika hifadhi ya Kitulo mkoani Njombe.

Aidha, barabara ya Ngomvi – Kimbiji hadi Pembamnazi yenye urefu wa (KM 27) upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika na sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza ujenzi huo.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete ametoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kuhakikisha inakuwepo miundombinu rafiki kwa walemavu ili kuwawezesha kutumia usafiri huo kwa urahisi.

Amesema kifungu cha 6(e) cha sheria ya LATRA Sura ya 413, kimeeleza kuwa moja ya majukumu ya LATRA ni kuhakikisha uwepo wa huduma ya usafiri wa umma unaoweza kutumiwa na watu wote wakiwemo wenye vipato vya chini ,waishio vijijini, wenye mahitaji maalum ambao inajumuisha watu wenye ulemavu.

Ameitaka LATRA kushirikiana na TBS katika kuweka na kusimamia utekelezaji wa viwango vya vyombo vya usafiri wa umma ili viwe na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu wakati wote.

Mhe. Mwakibete alikuwa akijibu swali la Mbunge Viti Maalum mkoa wa Iringa Dakta, Ritta Kabati alietaka kujua ni lini Serikali italeta sheria ya wamiliki wa vyombo vya usafiri kuwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

# NCHI ZA AFRIKA ZATAKIWA KUMILIKI MELI

Na **Redempta Ndubuja**



*Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi, Bw. Gabriel Migire akizungumza na Wadau wa usafiri kutoka Taasisi za Kikanda za Usafirishaji Majini (ISCOS), Jijini Dar es salaam.*

Nchi za Afrika zimetakiwa kuwekeza katika umilikiwa wa meli kubwa za kusafirisha mizigo kutoka nchi za Ulaya kuja Afrika kutoakana na ukauaji wa Biashara za Usafiri wa Majini duniani.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu anayesimamia Sekta ya Uchukuzi, Bw. Gabriel Migire kwenye mkutano uliowakutanisha wadau wa usafiri toka Taasisi ya kikanda inayohusu usafirishaji Majini (ISCOS).

"Usafiri kwa njia ya Maji ni mkubwa zaidi ya shehena ya Mizigo asilimia kumi duniani inasafirishwa kwa njia ya maji hivyo ni muhimu nchi za Afrika kumiliki meli ili tuweze kusafirisha mizigo", alisema Migire.

Aidha, Migire ameongeza kwa kusema kuwa serikali na watu binafsi wakimiliki meli itasaidia sana wanafunzi wanaosomea ubaharia katika vyuo vyetu watakuwa na nafasi kubwa ya kupata mafunzo na uzoefu katika meli hizo hivyo ni muhimu nchi zetu kuwa na meli kubwa.

Mwakilishi kutoka kampuni inayotengeneza Meli hapa nchini Songoro Marine Godwin Isdori amesema kuwa Biashara ya Usafiri kwa njia ya Maji ni kubwa hivyo ni Muhimu kwa Afrika kumiliki Meli kwani Biashara hiyo inatoa ajira kubwa kwa vijana.

Kwa upande wake, Katibu mtendaji wa wamiliki wa Meli Afrika Bi. Funmi Folorunso kutoka Nigeria amesema ni muhimu kwa Serikali na watu binafsi kumiliki meli kwani ni usafiri unaotegemewa sana na kutoa wito kwa watu binafsi na Serikali za Afrika kuhakikisha zinamiliki meli ili waweze kusafirisha mizigo na kuweza kupata pesa za kigeni katika nchi za Afrika.

Katibu Mtendaji wa Taasisi ya kikanda inayohusu usafirishaji Majini (ISCOS) Daniel Kiyange amesema kuwa ni muhimu kwa waafrika kuwa na meli kwani taasisi hiyo kwasasa inaangalia namna mzuri ya kushirikisha nchi wanachama kununua na kumiliki meli
Taasisi ya kikanda inayohusu Usafiri Majini( ISCOS) inajumuisha nchi za Tanzania, Burundi, Kenya, Uganda na Zambia.

# SINGIDA KUZALIWA UPYAA

Na **Christina Seggu**




*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akizungumza na wananchi wa Itigi (Hawapo Pichani), mara baada ya utiaji saini mkataba wa mradi wa Ujenzi wa Barabara za Maingilio katika Daraja la Sibiti, Noranga-Doroto na Itigi-Mkiwa, Mkoani Singida.*

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amesema Ujenzi wa Barabara za lami unaoendelea na utakaoanza hivi karibuni unalengo la kuufanya mkoa wa Singida kuwa kiunganishi na kitovu cha biashara kwa Mikoa ya kanda ya kaskazini, kati, ziwa na nyanda za juu kusini.

Akizungumza mjini Itigi katika hafla ya utiaji saini, mikataba ya ujenzi wa barabara za maingilio katika daraja la Sibiti zenye urefu wa KM 24.83 na barabara ya Makongolosi-Rungwa-Itigi-Mkiwa, sehemu ya Noranga hadi Doroto (KM 6) na Itigi hadi Mkiwa (KM25.569) kwa kiwango cha lami, Profesa Mbarawa amewataka wakazi wa Mkoa wa Singida kujipanga kutumia fursa za miradi hiyo kujikwamua kiuchumi.
"Ujenzi wa Sehemu ya Noranga - Doroto na Itigi - Mkiwa ni Muendelezo wa juhudi za Serikali kuifungua barabara yote ya Makongorosi-Rungwa -Itigi hadi Mkiwa kwa kiwango cha lami, na hivyo kuinganisha Mikoa ya Singida na Mbeya kwa urahisi zaidi"amesema Profesa Mbarawa

Aidha, Profesa Mbarawa amewataka viongozi wa Mkoa wa Singida, kuwapa ushirikiano wa kutosha Mkandarasi China Henan International Cooperation Group Co. Ltd. (CHICO) na wataalamu wengine wanaojenga barabara hizo ili zikamilike katika ubora uliokusudiwa na mapema Zaidi.

"Viongozi wa Mkoa na wa TANROADS, hakikisheni vijana wa mkoa wa Singida wanapata kipaumbele katika kupata ajira kwenye miradi inayoendelea ili kuwawezesha kunufaika kwa kupata utaalamu na kukua kiuchumi". Amesisitiza Profesa Mbarawa.

Barabara hizo zitakapokamilika zitaunganisha Kirahisi Mikoa ya Singida, Simiyu, Shinyanga , Arusha, Dodoma na Tabora na kufanya mkoa wa Singida kunufaika na Shughuli za kilimo, utalii na biashara.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila amesema kuwa barabara za Maingilio katika daraja la sibiti zitakapokamilika zitaondoaa adha ya usafiri katika daraja la hilo na hivyo kuvutia wasafirishaji wengi kupita njia hiyo.

Eng. Mativila ameongeza kuwa ujenzi huo utahusisha upanuzi wa makaravati makubwa na madogo na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua kwenye sehemu zenye mmomonyoko wa udongo.

Naye, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mhe Yahaya Masare akizungumza kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Singida, ameishukuru Serikali kwa namna inavyotekeleza Miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara mkoani humo,

Barabara ya itigi hadi Mkiwa ni Sehemu ya barabara itokayo Mbeya kupitia Makongorosi-Rungwa-itigi hadi Mkiwa yenye urefu wa Kilomita 413 ambapo sehemu ya Mbeya-Lwanjilo hadi Chunya (KM 72), na Chunya - Mkongorosi (KM 39), tayari imekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Katika hatua nyingine, Profesa Mbarawa amesema tayari Serikali imeshapata mkandarasi atakayejenga Barabara ya Handeni-Kibirashi hadi Singida (KM 462) na maandalizi ya kusaini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Arusha-Kongwa Junction (KM 438), Mbulu-Hydom (KM 400), na Ifakara-Lupilo-Malinyi hadi Namtumbo (KM.480 ) yatakamilika Mwezi juni mwaka huu.



*Aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila, akitoa taarifa ya mradi kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa (Hayupo pichani) katika hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi wa Ujenzi wa Barabara za Maingilio katika Daraja la Sibiti, Noranga-Doroto na Itigi-Mkiwa, Mkoani Singida*



*Baadhi ya Viongozi Wakishuhudia utiaji saini mkataba wa mradi wa Ujenzi wa Barabara za Maingilio katika Daraja la Sibiti, Noranga-Doroto na Itigi-Mkiwa, Mkoani Singida*



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila na Mwakilishi kutoka kampuni ya China Henan International Cooperation Group Co. Ltd. (CHICO), wakisaini mikataba wa mradi wa ujenzi wa barabara za maingilio katika Daraja la Sibiti, Noranga-Doroto na Itigi-Mkiwa, Mkoani Singida.*



*Baadhi ya Wananchi  Wakishuhudia utiaji saini mkataba wa mradi wa Ujenzi wa Barabara za Maingilio katika Daraja la Sibiti, Noranga-Doroto na Itigi-Mkiwa, Mkoani Singida*

# BANDARI KAVU YA KWALA MAMBO YAMEIVA

Na **Juhudi Mmari**



*Naibu katibu Mkuu, Sekta ya Uchukuzi, Dkt. Ally Possi, akizungumza na wafanyabishara na Watumishi wa Bandari, Wizara , TRC na TRA, (hawapo pichani) katika kuboresha utendaji kazi wa Bandari ya Dar es Salaam.*

Naibu katibu Mkuu Sekta ya Uchukuz, Dkt Ally Possi amezitaka taasisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Reli (TRC) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha wanaweka Mazingira Rafiki kwa wafanyabiashara ili kuanza kutumia Bandari kavu ya kwala kwani kwasasa ujenzi wa Bandari hiyo umefikia asilimia 98.

Possi ameyasema hayo kwenye kikao kilichowakutanisha wafanyabishara wa Bandari, Wizara , TRC na TRA, katika kuboresha utendaji kazi wa bandari ya Dar es Salaam.

" Ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala umefikia asilimia 98 hivyo taasisi zote zinatakiwa ziwezeshwe kuhamia ili kupunguza Msongamano wa Mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam" alisema Dkt.Possi

Aidha, Dkt. Possi amezielekeza taasisi hizo kutoongeza gharama katika kusafirisha Mizigo kutoka Bandari ya Dar es Saalam Mpaka kwala, kwani kuongezeka kwa gharama kutaongeza wafanyabiashara kutotumia bandari hiyo.

Baadhi ya wafanyabiashara katika sekta ya Bandari wamesema kuwa wapo tayari kutumia Bandari ya Kwala kwani bandari hiyo itasaidia kupunguza Mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, hivyo wanaomba Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), kuendelea kusimaia mifumo ya utoaji huduma ili kusiwe na usumbufu. .

Naye Meneja Uendeshaji kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) Focus Sahani amesema tayari Shirika hilo limeshatenga Mabehewa pamoja na vichwa vya treni kwa ajili ya kuanza kusafirisha Mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Kwala.

Kwa upande wake Meneja Msimamizi wa Ujenzi wa Bandari hiyo Alexander Ndibalema amesema kuwa ujenzi wa miundombinu ya reli na Barabara ya Kilometa 15 kutoka Vigwaza mpaka Kwala umekamika hivyo Bandari hiyo ipo tayari kuanza kazi.

# SULUHU YA CHANGAMOTO MPAKA WA TUNDUMA KUPATIKANA

Na **Redempta Ndubuja**



*Katibu Mkuu wa Uchukuzi, Gabriel Migire akifafanua jambo katika Kikao cha Makatibu Wakuu, Wataalam na Wasafirishaji wa Tanzania na Zambia kilichofanyika Mkoani Songwe hivi karibuni.*

Tanzania na Zambia zimekubaliana kutatua changamoto za usafirishaji wa mizigo baina ya nchi hizo hususani foleni ya maroli katika eneo la Tunduma ili kupunguza gharama na muda kwa wasafirishaji.

Akizungumza mara baada ya kikao cha cha Makatibu Wakuu, Wataalam na Wasafirishaji mkoani Songwe, Katibu Mkuu Uchukuzi, Gabriel Migire amesema suluhu ya kupunguza foleni katika mpaka huo kutarahisisha shughuli za usafirishaji wa mizigo na hivyo kuruhusu mzigo kumfikia mlaji kwa wakati.

“Changamoto katika usafirishaji ziko nyingi lakini kwa mpaka huu changamoto kubwa ni foleni ambapo madereva hukaa muda mrefu, hali hii inaongeza sana gharama za usafirishaji hivyo kikao cheti cha siku mbili hapa lazima tutoke hapa na majawabu’ Amesema Katibu Mkuu Migire.

Katibu Mkuu Migire ameongeza kuwa kikao hicho cha nchi mbili kimehusisha wataalam na wasafirishaji ili kujadili kwa kina changamoto zote ili kufanya wasafirishaji wengi zaidi kutumia mpaka huo wa Tunduma bila usumbufu.

Aidha, Katibu Mkuu Migire ameogeza kuwa moja ya makubaliano yaliyoafikiwa katika kikao hicho ni pamoja kuboresha sehemu za maegesho ya magari kwa pande zote mbili ili kurahisisha uingiaji na utokaji wa magari mpakani.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi na Logistic kutoka Zambia Mwalusaka Fredrick amesema kwa upande wa Zambia kuna changamoto ya miundombinu wezeshi ikiwemo barabara, skana za kukagua mizigo na uhaba wa watumishi mpakani na kuahidi kuzitatua kwa haraka ili kutokwamisha jitihada zinazoendelea za kurahisisha usafirishaji mpakani hapo.

Naye Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam Mrisho Mrisho amesema suluhu ya changamoto za mpaka wa Tunduma zitaongeza ufanisi katika bandari ya Dar es Salaam kwani mzigo utapakuliwa na kuondoka bandari hapo na kuwafikia walaji kwa wakati.

# TOLEO MAALUM

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

www.mwt.go.tz

Tanzania





# HISTORIA MPYA MIUNDOMBINU YA KIMKAKATI KUANDIKWA

**MEI 22 - 23, 2023 BUNGENI - DODOMA, TANZANIA**

#UtekelezajiWUU2022/23

Soma Kupitia Tovuti ya
Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi

# SERIKALI KUUNGANISHA WILAYA ZOTE NA MIKOA KWA LAMI

Na **Deniza Cyprian**




*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya, akizungumza na wananchi wa Haydom (Hawapo Pichani), mara baada ya utiaji saini mkataba wa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Labay-Haydom km 25, Mkoani Manyara.*

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amesema katika kuhakikisha uchumi jumuishi unafikiwa kwa watanzania wengi Serikali imedhamiria kuziunganisha wilaya zote nchini na makao makuu ya mikoa kwa barabara za lami.

Amesema hayo mjini Haydom wakati akishuhudia utiaji saini wa ujenzi wa barabara ya Labay-Haydom KM 25 ambayo ujenzi wake unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Naibu Waziri Kasekenya amebainisha kuwa nia ya serikali ni kuboresha mtandao wa barabara za uhakika na hivyo kuongeza ufanisi katika sekta ya usafiri na usafirishaji na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi kwa wananchi.

Barabara ya Labay-Haydom km 25 ni sehemu ya barabara kuu inayounganisha mikoa ya arusha-manyara-singida na simiyu hivyo kukamilika kwake kutaunganisha kwa urahisi mikoa ya kanda ya kaskazini na ile ya kanda ya ziwa na hivyo kurahisisha shughuli za usafiri.

“Barabara hii itakapokamilika itahuisha shughuli za kilimo,ufugaji,utalii na biashara na kuchochea uchumi”, amesema Naibu Waziri Kasekenya.

Mtendaji Mkuu wa Barabara nchini (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila amesema mradi huo unatekelezwa kwa utaratibu wa sanifu na kujenga ili kurahisisha utekelezaji wake.

Amesema zaidi ya shilingi bilioni 42 zitatumika katika ujenzi wa sehemu ya Labay-Haydom KM 25 na Mkandarasi JIANGXI GEO-ENGINEERING GROUP Limited kutoka China ndiye aliyeshinda zabuni hiyo na ujenzi utatumia miezi 18.




*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila pamoja na Mwakilishi wa kampuni ya Mkandarasi JIANGXI GEO-ENGINEERING GROUP Limited kutoka China wakionesha mikataba ya mradi wa Ujenzi wa barabara ya Labay-Haydom km 25, Mkoani Manyara.*



*Baadhi ya Wananchi wa mkoa wa Manyara, wakishuhudia utiaji saini mkataba wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Labay-Haydom km 25, Mkoani Manyara.*

# BARABARA ZA EPC + F HAZITALIPIWA

Na **Christina Seggu**




*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Eng. Mohamed Besta (wa pili kushoto waliokaa) na Mmoja wa Makandarasi kati ya wanne aliyepata kazi ya ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa EPC+ F, wakisaini mkataba wa utekelezaji wa miradi hiyo, Jijini Dodoma. Waliosimama ni baadhi ya Wabunge wakishuhudia.*

Serikali imesema kuwa utekelezaji wa miradi saba ya ujenzi wa barabara kwa njia ya EPC+ F haitalipiwa na wananchi watakaotumia barabara hizo kama ambavyo baadhi ya wananchi wanavyodhani.

Kauli hiyo imetolewa jijini Dodoma na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa, wakati wa utiaji saini wa miradi hiyo ambayo inatarajiwa kutekelezwa katika Kanda za Kaskazini na Kusini na kujengwa na makandarasi wanne (4).

"Tanzania haina barabara za kulipia mpaka sasa, hivyo upotoshaji unaosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kulipia kwenye barabara hizi si sahihi kwani barabara hizi ni za kawaida 'high way' kama zilivyo barabara nyingine" amesema Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa amesisitiza kuwa mradi huu ni wa kwanza na mkubwa kutekelezwa nchini kwani utapita katika mikoa 13 na lengo likiwa ni kuboresha mtandao wa barabara nchini na kuongeza ufanisi katika sekta ya usafiri na usafirishaji ili kuchochea uzalishaji katika maeneo zinapopita barabara hizi na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

"Barabara zitazojengwa zitapita katika mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Arusha, Manyara, Dodoma, Tanga, Singida, Mbeya, Songwe, Lindi, Mtwara, Simiyu na Iringa na hivyo zitarahisisha usafiri wa wananchi na usafirishaji wa mazao ya misitu, biashara, chakula, uvuvi na ufugaji, malighafi za madini kama vile makaa ya mawe, grafaiti na Chuma", amefafanua Waziri Mbarawa.

Aidha, Prof. Mbarawa ametaja miradi itakayotekelezwa kuwa ni ujenzi wa barabara ya Kidatu - Ifakara - Lupiro - Malinyi - Kilosa Mpepo - Londo - Lumecha/Songea (km 435.8) , Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa (km 453.42), Handeni - Kiberashi - Kijingu - Njoro - Olboroti Mrijo Chini - Dalai - Chambalo - Chemba - Kwa Mtoro – Singida (km 384.33), Igawa - Songwe – Tunduma (km 237.9), Masasi - Nachingwea - Liwale (km 175), Karatu - Mbulu - Hydom - Sibiti River - Lalago – Maswa (km 339) na barabara ya Mafinga - Mtwango – Mgololo (km 81).



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akizungumza na Viongozi pamoja na watumishi mbalimbali (hawapo Pichani), mara baada ya utiaji saini mikataba saba ya Ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa EPC+ F, Jijini Dodoma.*



*Baadhi ya Viongozi na Watumishi wa Sekta ya Ujenzi, wakishuhudia utiaji saini mikataba saba ya ujenzi wa barabara saba kwa utaratibu wa EPC+ F, uliofanyika Jijini Dodoma.*

> "
>
> Katika ujenzi wa barabara ya Igawa – Tunduma mkoani Mbeya Serikali imeamua kuijenga kwa njia nne ambapo barabara moja kati ya hizo itatumiwa na wasafirishaji wa malori tu ili kupunguza msongamano wa magari uliopo sasa katika eneo la Tunduma.

**Prof. Makame Mbarawa**
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*

Prof. Mbarawa amebainisha faida nyingine ya utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo kuchochea kiu ya matumizi ya bandari zetu kwa nchi jirani za Zambia, Malawi, Zimbabwe, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Pia ametaja kuwa barabara hizo zitatoa ajira za moja kwa moja kwa watanzania takriban 20,300 pamoja na kuwajengea uwezo wahitimu wa vyuo vikuu kwa masharti ya mikataba ya ujenzi na usimamizi ambapo wahitimu wasiopungua 70 watapata ajira.

Prof. Mbarawa ameiagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kushirikiana na Bodi ya Usajili ya Makandarasi (CRB) kuandaa wahandisi washauri wazawa watakaokuwa na uwezo na weledi wa kusimamia miradi mbalimbali ya ujenzi inayotekelezwa nchini.



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Eng. Mohamed Besta, akitoa taarifa ya mradi kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa (hayupo pichani) katika hafla ya utiaji saini mikataba Saba ya Ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa EPC+ F, Jijini Dodoma*



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Eng. Mohamed Besta na Mmoja wa Makandarasi kati ya wanne aliyepata kazi ya ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa EPC+ F, wakionesha mkataba wa utekelezaji wa miradi hiyo mara baada ya kusaini, Jijini Dodoma*

Awali akitoa taarifa ya miradi hiyo, Mtendaji Mkuu wa TANROADS Mhandisi Mohamed Besta, ameeleza kuwa jumla ya makandarasi 129 walionesha nia ambapo mchakato wa zabuni ulipitia hatua mbalimbali na hatimaye makandarasi wanne walikidhi vigezo vilivyowekwa.

"Makandarasi watakuwa timu nne kwa kila mradi mkubwa ambapo sehemu zote zitaanza kutekelezwa sambamba kwa wakati mmoja ili kuharakisha utekelezaji wa miradi hii" "amesisitiza Mha. Besta.

Ameongeza kuwa kupitia utaratibu huo makandarasi watawajibika kufanya usanifu wa kina na kujenga barabara hizo kwa viwango na ubora ulioainisha kwenye mkataba na huku vihatarishi vyote vinavyohusu usanifu wa mradi na muda wa ujenzi vitabebwa na mkandarasi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Selemani Kakoso, amesema kuwa kwa mara ya kwanza Tanzania inaandika historia ya kujenga barabara (Km 2,035) kwa mara moja wakati hapo awali Serikali ilikuwa inajenga Kilometa 200 hadi 250 kwa mwaka.

Utiaji saini wa mikataba Saba ya miradi ya ujenzi wa Barabara umefanywa na Serikali kupitia TANROADS na Kampuni ya China Civil Engineering Construction (CCECC), Sinohydro Cooperation, China Overseas Engineering Group (COVEC) na China Railway 15th Group kwa gharama ya Trioni 3.7.

# DARAJA LA JP MAGUFULI KUPUNGUZA UMBALI WA KM 210

Na **Segolena Francis**



*Daraja la JP Magufuli (kigongo - Busisi), mkoani Mwanza.*

Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, amesema ujenzi wa Daraja la JP Magufuli (Kigongo - Busisi) utakapokamilika utaokoa muda wa safari wa kutoka Mwanza kwenda Geita umbali wa kilometa 90 tofauti na sasa ambapo wanatumia umbali wa km 210 kupitia Kahama.

Amesema hayo mkoani Mwanza wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa daraja hilo ambalo limefikia zaidi ya asilimia 72 ya utekelezaji wake na kutoa fursa za ajira 1,001.

Ameeleza kuwa Daraja hilo likikamilika linatarajiwa kugharimu Tsh. Bilioni 716, ambapo itakuwa ni kama lango la kuingilia Mwanza kutokea mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma.
Amesisitiza kuwa ujenzi daraja hilo umezingatia viwango vya juu, linaweza kuwa imara kwa zaidi ya miaka 100.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima ametoa wito kwa wananchi waliopata fursa ya ajira katika mradi huo kutouhujumu kwa kuiba vifaa mbalimbali na kuiongezea Serikali gharama za ujenzi kwani hawamuibii mkandarasi bali wanawaibia watanzania wenzao.

“Tukimkuta mtu ambaye ana vifaa vinavyotokana na mradi huu tutafunga duka na hatafanya tena biashara Mwanza na tutamfungulia kesi ya uhujumu uchumi kisha atatueleza anaoshirikiana nao”, amesisitiza Mkuu wa Mkoa.

Ameeleza umuhimu wa Daraja hilo kuwarahisishia watalii wanaopitia Mwanza kutumia muda mchache kuvuka na kufanya utalii, hivyo daraja hili litarahisisha mawasiliano na kukuza sekta ya utalii.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya Daraja hilo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila, amesema daraja hilo lina umuhimu kwa wananchi wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa jumla, mfano kufika Mwanza kwenda Geita au Sengerema ilikuwa ni lazima uzunguke hadi Kahama, hivyo Daraja la Busisi litaondoa mzunguko huo.

“Daraja hili litaunganisha watu wa Mwanza, Geita, Kagera na Nchi jirani ya Uganda, kwa huo ukaribu utatumia muda mfupi kwenda nchi nyingine zinazotuzunguka kama Rwanda”amesema Eng. Mativila.

Ameeleza kuwa daraja hilo lilianza kujengwa Mwaka 2020 baada ya mkataba kusainiwa Mwaka 2019 na makubaliano ya mkataba ni kukamilika Februari 25, 2024 kulingana na makubaliano yaliyopo na mkandarasi anafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha wanafikia lengo hilo.

# PROF. MBARAWA: HAKUNA MIRADI YA UJENZI KUSIMAMA

Na **Deniza Cyprian**



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akifafanua jambo kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendinga, wakati wakikagua hatua za ujenzi wa barabara ya Ntendo – Kizungu (km 25) kwa kiwango cha lami, mkoani humo.*

Serikali imewaagiza wakandarasi wanaotekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege kuhakikisha wanaendelea na utekelezaji wa miradi hiyo ili ikamilike kwa viwango na kwa muda uliopangwa.

Agizo hilo limetolewa mkoani Rukwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, wakati akikagua utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 179) awamu ya kwanza inayoanzia Ntendo - Kizungu (km 25) kwa kiwango cha lami.

Amesisitiza kuwa kuhusu suala la malipo Serikali inatambua na itaendelea kuhakikisha inakamalisha taratibu za malipo mara tu baada ya wakandarasi kuwasilisha hati za madai.

"Serikali inapokea madai ya wakandarasi na kuna taratibu za uhakiki ilizojiwekea ili kujiridhisha hivyo TANROADS endeleni kuwasimamia wakandarasi wote nchini tuikamilishe miradi", amesisitiza Prof. Mbarawa.
Aidha, amesema hivi karibuni Serikali itaweka historia kwa kusaini mikataba ya EPC + F ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 2,000 kwa ajili ya kuunganisha mikoa yote kwa kiwango cha lami.

Awali akitoa taarifa ya mradi, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila, ameeleza mkataba wa ujenzi wa mradi huo umetolewa kwa kampuni ya China Geo - Cooperation ya nchini China ambapo mkataba ulisainiwa tarehe 29 Machi 2022 na mradi ulianza tarehe 6 Juni 2022 kwa muda wa miezi 18 pamoja na miezi 12 ya matazamio.

Kuhusu utekelezaji wa mradi huo, Meneja wa TANROADS, mkoa wa Rukwa Eng. Mgeni Mwanga, amesema mradi huo utajumuisha ujenzi wa makalvati makubwa 17 na makalvati madogo 43 ambapo hadi sasa makalvati makubwa 4 yamekamilika na 9 ujenzi unaendelea huku makalvati madogo 5 yamekamilika na yaliyobakia yanaendelea.


Ameongeza kuwa kwa ujumla utekelezaji wa barabara hiyo umefikia asilimia 23 na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2023.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendinga amesema kuwa barabara hiyo ni muhimu sana kwani inapita kwenye maeneo yenye fursa mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji wa madini (makaa ya mawe) na uchimbaji wa gesi.

"Hii barabara ikikamilika tutakuwa na usafiri wa uhakika wa bidhaa na mazao yetu tunayolima kutoka katika Bonde la Ziwa Rukwa hadi kufkia Sumbawanga mjini ambako ndiko soko la bidhaa zinazozalishwa linapatikana", amefafanua Mkuu wa Mkoa huyo.

Naye Mbunge wa jimbo la Sumbawanga Mjini, Aeshi Hillary ameishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele miradi ya ujenzi inayoendelea katika jimbo lake na mkoa kwa ujumla.

Amesema wasafiri wa mazao na bidhaa wamekuwa wakipata adha kya usafirishaji kwani barabara hiyo inapita kwenye miinuko na kona kali hali ambayo inasababisha magari makubwa kuzunguka kupitia miji ya Majimoto-Kibaoni-Katete-Kizi hadi Sumbawanga umbali wa takribani kilometa 230 ukilinganisha na kilometa 37 za kupitia hapa Ntendo - Muze kama hali ya barabara ikikamilika.



*Muonekano wa sehemu ya ujenzi wa barabara ya Ntendo – Kizungu (km 25) kwa kiwango cha lami, mkoani Rukwa. Ujenzi wa barabara hiyo unatekelezwa na kampuni ya China Geo – Engineering Corporation kwa gharama ya shilingi Bilioni 45.299 kwa muda wa miezi 18.*



*Kazi zikiendelea za ujenzi wa moja ya makalvati katika barabara ya Ntendo – Kizungu (km 25) inayojengwa kwa kiwango cha lami, mkoani Rukwa.*

Barabara ya Ntendo - Muze - Kilyamatundu (km 179) ni moja ya barabara muhimu inayounganisha mikoa ya Songwe, Rukwa, Katavi kupitia Bonde la Ziwa Rukwa.

# WADAU WA BANDARI WAASWA KUTUMIA FURSA KUBORESHA HUDUMA ZA USAFIRI

Na **Redempta Ndubuja**



*Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Aron Kisaka akizungumza na Wadau wa Bandari ya Ziwa Viktoria (hawapo pichani) wakati alipofungua kikao cha kwanza cha wadau hao, kilichofanyika jijini Mwanza.*

Serikali imewataka wadau wa bandari kutumia vyema fursa za vikao vinavyofanyika mara moja kwa mwezi ili kuja na suluhu na mikakati madhubuti ya kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji nchini katika Ziwa Viktoria.

Akizungumza katika kikao cha kwanza cha wadau wa maboresho ya bandari jijini Mwanza, Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Mhandisi Aron Kisaka, amesema kukutana pamoja kutawawezesha wadau kuwasilisha taarifa za utendaji zinazoeleza mipango, mikakati na changamoto na namna ya kukabiliana na changamoto ili kuwa na uelewa wa pamoja.

“Napenda kuwashukuru kwa kushiriki katika kikao hiki na niwatake kuhakikisha yale yote tunayozungumza hapa tujiwekee na ukomo ili vikao vinavyofuata tujipime kama tunakwenda mbele au changamoto hizo ziende kwa mamlaka nyingine kwa maamuzi’ amesema Mhandisi Kisaka.

Mhandisi Kisaka amewataka wadau muhimu kama Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Nchini (TPA), Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) na Wamiliki wa Bandari zilizorasimishwa Mkoani Mwanza kutafuta masoko kwa nchi Jirani zinazotumia bandari za Kanda ya Ziwa ili kupata mzigo mwingi zaidi na kuinua pato la taasisi hizo na wananchi kwa ujumla.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa MSCL, Eric Hamis ameipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa meli lengo likiwa kuhakikisha kuna mazingira mazuri ya usafiri na usafirishaji katika Ziwa Viktoria.

Naye Meneja wa Bandari ya Mwanza Ferdinand Nyathi, amesema kupitia vikao hivi mipango mbalimbali ya wadau itawasilishwa kwa wadau ili kuwa na uelewa wa pamoja ambao matokeo yake itakuwa ni kuboresha miundombinu kwa utaratibu mzuri ambao tija yake itakuwa ni kuongeza pato la mamlaka, Taifa na mwananchi mmoja mmoja.

Meneja ameeleza mipango ya bandari ni kujenga gati maalum kwa bandari ya Mwanza, Kemondo na Kagera kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa zaidi ikiwemo ya MV Mwanza hapa kazi tu ambayo inakamilishwa.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) inaendelea na mpango wake wa kusimamia vikao vya wadau wa maboresho ya bandari katika Bandari za Bahari ya Hindi, na kwenye Maziwa nchini lengo ni kuhakikisha bandari zinaleta ufanisi na tija na hatimaye kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji nchini.

# DARAJA LA JP MAGUFULI KUPUNGUZA UMBALI WA KM 210

Na **Biseko Ibrahim**




*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhe. Atupele Mwakibete, akizungumza na Waandishi wa habari kuhusiana na maadhimisho ya siku ya hali ya hewa duniani inayoadhimishwa machi 23 kila mwaka, ambapo kwa mwaka huu kauli mbiu yake ilikua ni ,mustakabali wa hali ya hewa,tabia ya nchi na maji kwa vizazi vyote ,katika ukumbi wa idara ya habari maelezo jana, jijini Dodoma.*

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Atupele Mwakibete amewataka wadau wa kilimo, nishati, maji, mifugo, uvuvi na wananchi kwa ujumla kufuatilia kwa karibu taarifa za hali ya hewa zinazotolewa mara kwa mara na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ili kuweza kupanga na kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii.

Ametoa rai hiyo jijini Dodoma wakati wa maadhimisho ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani na kusema changamoto za tabia za nchi zimebadili majira na vipindi vya hali ya hewa hali inayoepekelea mabadiliko ya mara kwa mara ambayo bila kupata taarifa sahihi za hali ya hewa changamoto zitaongeeka hasa kwa wadau wa kilimo.

"Serikali imeamua kuhakikisha Sekta ndogo ya Hali ya Hewa inaimarika na taarifa zinadizi kuboreshwa ndio maana imetenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha rada zinafikia saba lengo ni ni kuwezesha uhakika wa taarifa kuongezeka". Amesema Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete ametoa rai kwa TMA kuhakikisha wanabuni mbinu mbalimbali ambazo zitafanya ya taarifa zinazotolewa kuweza kuwafikia wadau wakiwemo wakubwa na wadogo ili kuwafanya kuzitumia kwa shughuli zao za maendeleo.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Dkt. Ladislaus Chang'a amesema miongoni mwa juhudi zinazoendelea kufanywa kwenye utoaji wa elimu kwa umma ni pamoja na kufanya semina na warsha za mara kwa mara kwa waandishi wa Habari nchini ili kuwezesha wadau kupata taarifa kwa wakati.

Mkurugenzi Chang'a ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwekeza kwenye Miundombinu kwani kwa kuwezeshwa kuwa na rada saba kutapandisha uhakikisha usahihi wa taarifa za utabiri kufikia zaidi ya asilimia 85.

Siku ya hali ya hali Duniani huadhimishwa kila mwaka ifikapo Machi 23 ambapo Tanzania ambapo inaungana na nchi nyingine wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani (WMD) kauli mbiu ya mwaka huu imejikita uhamamsishaji wa matumizi sahihi ya maji ili kupunguza changamoto za tabia nchi zinazochangia mabadiliko makubwa ya hali ya hewa.

# SERIKALI YAAHIDI KUTATUA CHANGAMOTO ZA BARABARA YA NATA – SANZATE

Na **Deniza Cyprian**



*Muonekano wa sehemu ya barabara ya Sanzate – Nata (km 40), inayojengwa kwa kiwango cha lami, mkoani Mara.*

Serikali imewahakikishia wananchi wa Isenye, Wilaya ya Serengeti kuzimaliza changamoto zinazoukabili mradi wa ujenzi wa barabara ya Nata - Sanzate (km 40) kwa kiwango cha lami ili iweze kukamilika na kuondoa adha ya usafiri wanayoipata wananchi hao.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya wakati akijibu maswali ya wananchi na kuahidi kutoa ushirikano kwa mkandarasi kwa kuonesha maeneo yote yenye changamoto ili yaweze kutatuliwa kwa haraka pindi ujenzi wa barabara hiyo unapoendelea.

Wananchi hao wameeleza changamoto hizo kuwa ni pamoja na kusuasua kwa mradi na mkandarasi kutoweka mifereji ya kupitisha maji na hivyo kuathiri makazi ya watu.

"Siku zote unapohitaji maendeleo lazima kutakuwa na mabadiliko mengi ya utaratibu wa maisha yaliyokuwepo, na uwepo wa ujenzi wa barabara hii si kukomoa au kuonea watu bali ni kuleta manufaa makubwa na endelevu kwa jamii", amesisitiza Naibu Waziri Kasekenya

Aidha, amemuagiza mkadarasi kuongeza vifaa, rasilimali watu na kuongeza muda wa kazi hata kwa kufanya kazi usiku na mchana kwa kuwa wananchi wanahitaji kuona barabara hiyo ikiwa imekamilika.

"Tumemuagiza aongeze wafanyakazi, vifaa na ikiwezekana aongeze shift ili barabara hii ikamilike na ndio kilio cha wananchi hawa kuona barabara inakamilika", amesema Eng. Kasekenya.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Vicent Mashinji, amemshukuru Naibu Waziri Kasekenya kwa ujio wake katika mkoa huo kwani utaleta msukumo katika ujenzi wa miradi mingi inayoendelea hasa kwa barabara hiyo kwani ni kiungo muhimu kati ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda



*Naibu Waziri wa Ujenzi. Eng. Godfrey Kasekenya, akikagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Sanzate – Nata (km 40), kwa kiwango cha lami, mkoani Mara.*

ya Kaskazini na nchi jirani ya Kenya. Akijibu hoja ya wananchi kuhusu uwepo wa mifereji, Meneja wa Wakala ya Barabara (TANROADS) mkoa wa Mara, Eng. Vedastus Maribe, amesema changamoto hiyo anaifahamu na amekwisha muelekeza mkandarasi kusambaza vifusi vilivyowekwa katika maeneo hasa ya makazi ili kuzuia athari za maji kuingia ndani ya nyumba za watu.

Kuhusu mradi wa barabara hiyo, Eng. Maribe, ameeleza kuwa mradi huo mpaka sasa umefikia asilimia 32 na kazi zinazoendelea ni pamoja na kunyanyua tuta la barabara ambapo hadi sasa mkandarasi kafikisha km 23.4 na pia amekwishajenga madaraja madogo 45 kati ya 46, madaraja 11 kati 16 na madaraja makubwa kashajenga 1 kati ya 2 yanayotakiwa.

Ameeleza ujenzi wa barabara hiyo inayojengwa kwa gharama ya takribani Bilioni 39 na mkandarasi China Railway Seventh Group na kusimamiwa na Kitengo cha Usimamizi wa Miradi cha Wakala ya Barabara nchini (TANROADS) – TECU.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo amekagua na kuridhishwa na barabara ya Nyamuswa hadi Bulambwa (km 56.4) iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya takribani Bilioni 67 zote zikiwa ni fedha za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mradi huo ambao upo katika kipindi cha matazamia ya mwaka mmoja umetekelezwa na mkandarasi China Civil Engineering Construction Cooperation (CCECC) na kusimamiwa na kampuni ya Doch.
Barabara hiyo ni kiungo muhimu kati ya mikoa ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Kaskazini pamoja na Kisiwa cha Ukerewe.

# TANROADS YATEKELEZA KILOMETA 238.9 ZA BARABARA ZA LAMI

Na **Siti Said**



*Muonekano wa hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa Barabara ya Kazilambwa hadi Changu (KM 36) inayojengwa kwa kiwango cha Lami, Mkoani Tabora.*

Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Tabora imesema imejenga barabara zenye urefu wa kilometa 238.9 kwa kiwango cha lami ambazo zimegharimu zaidi ya bilioni 300 na hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi mkoani humo.

Akizungumza na waandishi wa habari Kaimu Meneja wa TANROADS mkoa wa Tabora, Mhandisi Rwegoshora Michael walipotembelea mradi wa ujenzi wa barabara ya Kazilambwa - Chagu (km 36) kwa kiwango cha lami ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 89.62 kwa gharama ya shilingi Bil 36.9 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mhandisi Rwegoshora amesema kuwa ujenzi wa barabara hiyo ukikamilika utaiunganisha mkoa wa Tabora na Kigoma kwa upande wa Tabora ambapo ndio kipande kilichobakia kuunganishwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ameeleza mradi huo unatekekelezwa na mikoa miwili ambapo kwa upande wa Tabora wanajenga kilometa 26 na kwa upande wa Kigoma wanatekeleza kilometa 10.

Ametaja miradi iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami mkoani humo ikiwemo barabara ya Tabora - Koga - Mpanda sehemu ya Usesula - Komanga yenye urefu wa kilometa 117.5 na barabara ya Nyahua - Chaya yenye urefu wa kilometa 85.4.

“Tunaishukuru Serikali kwa kutekeleza kwa vitendo sera yake ya kuunganisha mikoa na wilaya kwa barabara kwa kiwango cha lami maboresho hayo yana matokeo ya moja kwa moja kwani bidhaa nyingi zitawafikia walaji kwa wakati lakini huduma zitaboreka hususani usafirishaji”, amesema Kaimu Meneja.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Kigoma Mhandisi Ngoko Mirumbe amesema mradi huo ukikamilika utapunguza muda wa usafiri wa kilometa 300 kutokea Dar es Salaam.

"Zamani watu wa Kigoma walikuwa wanasafiri kwenda Mkoa wa Dar es Salaam kupitia Nyakanazi, kukamilika kwa mradi Dar es Salaam hadi Kigoma (kwa baadhi ya vipande vilivyobaki), zaidi ya kilometa 300 zitakuwa zimepungua, na hii litaleta unafuu kwa usafiri na gharama zitapungua", amefafanua Mhandisi Mirumbe.

Amesema barabara hiyo inajengwa na kampuni ya STECOL Corporation na kusimamiwa na Kitengo cha Usimamizi wa Miradi cha TANROADS - TECU.

Amesema kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutawezesha shughuli mbalimbali za usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria kati ya nchi ya Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Rwanda na hivyo kuchangia pakubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Ameongeza kuwa faida hiyo muhimu kiuchumi inatokana na kwamba ujenzi wa barabara hiyo utaiunganisha Mkoa wa Kigoma na Tabora huku ikitatua changamoto ya muda mrefu ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine nchini na hivyo kuwezesha kufika kwa urahisi katika nchi hizo.



*Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mkoa wa Tabora, Mhandisi Rwegoshora Michael akimsikiliza Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Mirumbe kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kazilambwa hadi Changu (KM 36) inayojengwa kwa kiwango cha Lami, Mkoani Tabora.*



*Mmoja wa mafundi wa Kampuni ya M/S Cotel akiendelea na kazi ya uwekaji wa miundombinu ya Barabara katika Barabara ya Kazilambwa hadi Changu (KM 36) inayojengwa kwa kiwango cha Lami, Mkoani Tabora.*

# BIL 234.5 KUUFUNGUA MKOA WA MTWARA KWA BARABARA ZA LAMI

Na **Segolena Francis**

Serikali imesaini mikataba miwili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Mnivata – Newala – Masasi (km 160) pamoja na ujenzi wa daraja la Mwiti yenye jumla ya shilingi Bilioni 234.512 kwa lengo la kuwaondolea wananchi wa Mtwara kero ya usafiri na usafirishaji.

Tukio hilo limefanyika wilayani Newala mkoani humo ambapo limeshuhudiwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa na viongozi wengine wa mkoa, wabunge na wananchi ambapo pamoja na mambo mengine Prof. Mbarawa amesema kuwa ujenzi wa barabara hiyo utaboresha mtandao wa barabara na madaraja katika ukanda wa Kusini.

Akizungumza na wananchi wa mkoa huo wakati wa hafla hiyo, Prof. Mbarawa ameeleza kuwa barabara hiyo itaboresha usafiri na usafirishaji wa malighafi za viwandani kama makaa ya mawe na saruji, mazao ya chakula na kilimo, mifugo, uvuvi, bidhaa za kibiashara na mazao ya misitu kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mtwara pamoja na mikoa jirani ya Lindi, Ruvuma na Pwani kwenda maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Prof. Mbarawa, amewaasa wananchi wa Mtwara kutoa ushirikiano kwa makandarasi waliopata kazi ya ujenzi wa barabara hiyo pamoja na kujiepusha na vitendo vya uhalifu katika miradi hiyo.

"Hakikisheni mnatoa ushirikiano kwa vijana mtakaopata kazi katika mradi huu, muache tabia ya wizi wa vifaa, mkifanya hivi mtasababisha miradi kukamilika kwa wakati", amesema Prof. Mbarawa.



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa akisisitiza jambo wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barbara ya Mnivata-Newala-Masasi (KM 160) pamoja na ujenzi wa Daraja la Mwiti iliyofanyika Wilayani Newala, Mkoani Mtwara.*

Waziri Prof. Mbarawa ameahidi kuendelea kuufungua mkoa wa Mtwara kwa kuunganisha mkoa wa Lindi na mikoa jirani kwa barabara za lami pamaoja na ujenzi wa reli na bandari.

"Nimepokea maombi ya barabara mbalimbali ikiwemo ya kuunganisha kwa lami barabara ya Newala-Mtama, Mtama-Tandahimba, Mtwara-Kilambo, Newala - Mbuyuni ambapo fedha zimetengwa na upembuzi yakinifu na usianifu wa kina unaendelea", amefafanua Prof. Mbarawa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Ahmed Abbas, amesema utekelezaji wa mradi huo unaunganisha wilaya zote za mkoa huo na hivyo kutaimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii na kupunguza gharama za maisha kwa mwananchi mmoja mmoja.


Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Eng. Mohamed Besta, amesema kuwa Mikataba hiyo imesainiwa kati ya Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), na

Kampuni ya China Wu Yi Co. Ltd sehemu ya kutoka Mnivata-Mitesa (Km 100), kwa gharama ya Shilingi Bilioni 141.964 na Kampuni ya China Communications Construction Co. Ltd atakayejenga sehemu ya pili kutoka Mitesa-Masasi (km 60) pamoja na ujenzi wa daraja la Mwiti kwa gharama ya Shilingi Bilioni 92.548.

Eng. Besta ameahidi kuwa Wakala utasimamia vyema wakandarasi hao kukamilisha barabara hiyo kwa viwango vya ubora.

Pia ameongeza kuwa mradi huo utakuwa na miradi ya nyongeza kwa jamii ambapo wakandarasi watajenga Zahanati, Stendi, Shule, Maghala ya kuhifadhia mazao, Magari ya Wagonjwa na ununuzi wa X-Ray.

Ujenzi wa barabara ya Mtwara-Newala-Masasi (km 160) ni moja ya mkakatinwa Serikali wa kuboresha mtandao wa barabara hapa nchini na ni kiungo muhimu kwa barabara kuu ya kutoka Mtwara mpaka Mbamba bay inayojulikana kama Ushoroba wa Mtwara (Mtwara corridor) ambayo inaunganisha na nchi jirani ya Msumbiji.



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Eng. Mohamed Besta (kushoto) na Muwakilishi wa Kampuni China Communications Contruction Company wakisaini mkataba wa utekelezaji wa ujenzi wa barabara sehemu ya Mitesa hadi Masasi (KM 60) kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Daraja la Mwiti, Mkoani Mtwara.*




*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Eng. Mohamed Besta (kushoto) na Muwakilishi wa Kampuni ya China Wu Yi Company wakionesha mkataba wa utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya sehemu ya Mnivata-Mitesa (KM 100) mara baada kuisaini Wilayani Newala, Mkoani Mtwara.*



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa akizungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Kazi Maalum, Kapteni Mstaafu John Mkuchika, wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barbara ya Mnivata-Newala-Masasi (KM 160) pamoja na ujenzi wa Daraja la Mwiti iliyofanyika Wilayani Newala, mkoani Mtwara.*




*Mkurugenzi Msaidizi Barabara Kuu kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) Mhandisi Light Chobya, akimsikiliza Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa (hayupo pichani) wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Mnivata-Newala-Masasi (KM 160) na ujenzi wa Daraja la Mwiti iliyofanyika Wilayani Newala, Mkoani Mtwara.*



*Sehemu ya Watumishi wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) wakimsikiliza Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa (hayupo pichani) wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barbara ya Mnivata-Newala-Masasi (KM 160), pamoja na ujenzi wa Daraja la Mwiti Wilayani Newala, Mkoani Mtwara.*

# KIWANJA CHA NDEGE - SUMBAWANGA KUBORESHWA

Na **Shukuru Senkondo**



**PICHANI:** *Muonekano wa sehemu ya barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha changarawe katika Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga ambapo Serikali imesaini mkataba wa ukarabati na upanuzi wa kiwanja hicho kwa gharama ya shilingi Bilioni 55.908, mkoani Rukwa. Ukarabati wa barabara hiyo utafanyika kutoka kilometa 1,516 hadi kufikia kilometa 1,750 kwa kiwango cha lami.*

Mkoa wa Rukwa waingia katika historia mpya mara baada ya Serikali kupitia Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS) kuingia mkataba na Kampuni ya M/s Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd ya nchini China kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga kwa gharama ya Shilingi Bilioni 55.908 kwa muda wa miezi 18.

Uboreshaji huo ni utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii Mkoani humo na ukanda wa Magharibi mwa nchi ya Tanzania ili kuongeza ufanisi katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Zoezi la utiaji saini wa mkataba huo uliofanyika katika Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga, mkoani humo umefanyika kati ya Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Matavila pamoja na Mwanasheria wa TANROADS, Wakili Gurisha Mwanga na kushuhudiwa na wananchi, viongozi mbalimbali wa Serikali na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa.

Akizungumza baada ya Zoezi hilo, Prof. Mbarawa ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuboresha miundombinu pamoja na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huo.

Waziri Prof. Mbarawa ameeleza kuwa uboreshaji wa kiwanja hicho utakapokamilika utaruhusu kiwanja hicho kufanya kazi saa 24 yaani usiku na mchana na kitakuwa na uwezo wa kupokea ndege aina ya Boeing Q 400 pamoja na ATR 72.

Amesema utekelezaji wa mradi huo umeletwa mahsusi ili kuchochea shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, utalii, uwekezaji, uvuvi, usafirishaji wa mizigo na abiria na shughuli za kijamii kwa ujumla.
“Mapema mwakani wana Sumbawanga mtegemee ndege ya kwanza kutua hapa”, amesisitiza Prof. Mbarawa.

Mkoa wa Rukwa waingia katika historia mpya mara baada ya Serikali kupitia Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS) kuingia mkataba na Kampuni ya M/s Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd ya nchini China kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga kwa gharama ya Shilingi Bilioni 55.908 kwa muda wa miezi 18.

Uboreshaji huo ni utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii Mkoani humo na ukanda wa Magharibi mwa nchi ya Tanzania ili kuongeza ufanisi katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Zoezi la utiaji saini wa mkataba huo uliofanyika katika Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga, mkoani humo umefanyika kati ya Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Matavila pamoja na Mwanasheria wa TANROADS, Wakili Gurisha Mwanga na kushuhudiwa na wananchi, viongozi mbalimbali wa Serikali na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa.

Akizungumza baada ya Zoezi hilo, Prof. Mbarawa ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuboresha miundombinu pamoja na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huo.

Waziri Prof. Mbarawa ameeleza kuwa uboreshaji wa kiwanja hicho utakapokamilika utaruhusu kiwanja hicho kufanya kazi saa 24 yaani usiku na mchana na kitakuwa na uwezo wa kupokea ndege aina ya Boeing Q 400 pamoja na ATR 72.

Amesema utekelezaji wa mradi huo umeletwa mahsusi ili kuchochea shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, utalii, uwekezaji, uvuvi, usafirishaji wa mizigo na abiria na shughuli za kijamii kwa ujumla.
“Mapema mwakani wana Sumbawanga mtegemee ndege ya kwanza kutua hapa”, amesisitiza Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa amefafanua kuwa uboreshaji wa kiwanja hicho pia utahusisha ujenzi wa jengo jipya la abiria, ununuzi na usimikaji wa taa za kuongozea ndege (AGL) na mitambo ya Usalama (DVOR/DME), barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari na uzio wa usalama.

Aidha, amesema kiwanja hicho kwa sasa kina barabara ya kuruka na kutua ndege ya kiwango cha changarawe yenye urefu wa kilometa 1,516 na upana wa meta 30 ambapo kupitia mradi huu barabara hiyo itaboreshwa kufikia urefu wa kilometa 1,750 na upana wa meta 30 kwa kiwango cha



*Aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila akisaini mkataba wa ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbwanga na Mwakilishi kutoka kampuni ya M/s Beijing Construction Engineering Group ya nchini China kwa gharama ya Bilioni 55.908 kwa muda wa miezi 18, mkoani Rukwa.*




Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akizungumza na wananchi wa mkoa wa Rukwa mara baada ya kusiani mkataba wa ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbwanga utakaogharimu kiasi cha shilingi Bilioni 55.908, mkoani humo.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akizungumza na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendinga, ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara katika hafla ya utiaji saini mkataba wa ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbwanga utakaogharimu kiasi cha shilingi  Bilioni 55.908, mkoani humo.

# TAKRIBANI BILIONI 77 KUBORESHA MIUNDOMBINU YA SENGEREMA

Na **Siti Said -** WUU




*Aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Eng. Rogatus Mativila, akisaini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Sengerema - Nyehunge (km 54.4) kwa kiwango cha lami na Mwakilishi kutoka kampuni ya AVM - Dilingham kwa gharama takribani Bilioni 73. mkoani Mwanza. Barabara hiyo ni sehemu ya mtandao wa barabara inayounganisha Mkoa wa Mwanza na Mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma.*

Serikali imesaini mikataba miwili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ya Sengerema - Nyehunge (km 54 4), kwa kiwango cha lami na ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya maeneo ya Buyagu - Mbalika katika wilaya ya Sengerema na Misungwi kwa gharama ya takriban kiasi cha Bilioni 77 mkoani Mwanza.

Mkataba wa barabara umesainiwa kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), na kampuni ya AVM - Dilingham ya Uturuki kwa gharama ya shilingi Bilioni 73 na mkataba wa kivuko kipya umesainiwa kati ya Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na kampuni ya Songoro Marine kwa gharama ya Bilioni 3.8.

Akishuhudia utiaji saini mikataba hiyo mkoani humo, Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya, amesema kuwa miradi hiyo itakapokamilika itaimarisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi waishio maeneo ya Wilaya ya Sengerema hasa Halmashauri ya Buchosa.

Aidha, amesema miradi hiyo itasaidia kutengeneza ajira kwa wananchi wa Wilaya hiiyo wakati wa utekelezaji wa ujenzi.

Eng. Kasekenya ameziagiza TANROADS na TEMESA kuisimamia vyema miradi yote hiyo ili thamani ya fedha ipatikane na kukamilika kwa wakati.

Ameeleza kuwa ujenzi wa barabara na kivuko hicho utatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani kwa asilimia 100 ikiwa ni moja ya juhudi na mikakati ya Serikali chini ya Uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan katika kuboresha maisha ya wananchi wake hususan wana Sengerema.

Akiongelea kuhusu barabara Eng. Kasekenya ameeleza kuwa barabara hiyo ni sehemu ya mtandao wa barabara muhimu za nchi yetu ambayo inaunganisha Mkoa wa Mwanza na Mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma.



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akihutubia wananchi wakati wa utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Sengerema - Nyehunge (km 54.4) kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Kivuko kipya cha Buyagu – Mbalika, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza.*

“Barabara hii itakapokamilika itachochea shughuli za kiuchumi kama vile usafirishaji wa bidhaa mbalimbali na abiria, bidhaa za uvuvi, mazao ya chakula, mazao ya biashara mazao ya misitu na shughuli za kijamii kwa ujumla”, amesema Eng. Kasekenya.

Eng. Kasekenya ametaja miradi mingine ya madaraja na barabara ambayo ujenzi/ukarabati wake unaendelea kwa kugharamiwa na Serikali ni ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi lenye urefu (mita 3,000) pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66, barabara ya Tarime – Mugumu, sehemu ya Tarime hadi Nyamwaga (km 25), barabara ya Bugene hadi Burigi Chato National Park (km 60), Daraja la Kitengule lenye urefu wa mita 140 pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 18, barabara ya Nyamuswa - Bunda - Kisorya hadi Nansio sehemu ya Nyamuswa – Bunda hadi Bulamba (km 56.4), na barabara ya Makutano – Nyamuswa hadi Ikoma Gate sehemu ya Sanzate hadi Natta (km 40).

Kwa upande wa ujenzi wa kivuko kipya Eng. Kasekenya amesema kuwa kivuko hicho kitatoa huduma Buyagu na Mbalika katika Wilaya ya Sengerema na Misungwi lengo likiwa ni kuwapatia usafiri ulio salama na wenye uhakika wananchi wa maeneo hayo ambayo wamekuwa wakitumia mitumbwi kwenye eneo hilo lenye umbali wa takribani kilometa saba.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Eng. Rogatus Mativila, amesema kuwa zabuni za ujenzi wa barabara hiyo zilitangazwa tarehe 13 Juni, 2022 na kufunguliwa tarehe 30 Agosti, 2022 ambapo jumla ya zabuni12 zilipokelewa na kufanyiwa tathmini na Mkandarasi aliyeshinda tuzo ni Kampuni ya AVM-Dilingham Construction International Inc. ya nchini Uturuki kwa muda wa miezi 28.

Serikali imesaini mikataba miwili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ya Sengerema - Nyehunge (km 54 4), kwa kiwango cha lami na ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya maeneo ya Buyagu - Mbalika katika wilaya ya Sengerema na Misungwi kwa gharama ya takriban kiasi cha Bilioni 77 mkoani Mwanza.

Mkataba wa barabara umesainiwa kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), na kampuni ya AVM - Dilingham ya Uturuki kwa gharama ya shilingi Bilioni 73 na mkataba wa kivuko kipya umesainiwa kati ya Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na kampuni ya Songoro Marine kwa gharama ya Bilioni 3.8.

Akishuhudia utiaji saini mikataba hiyo mkoani humo, Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya, amesema kuwa miradi hiyo itakapokamilika itaimarisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi waishio



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Bw. Lazaro Kilahala.*



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Bw. Lazaro Kilahala na Meneja wa Kampuni Songoro Marine, Major Songoro wakionesha mkataba wa ujenzi wa kivuko kipya cha Buyagu – Mbaika mara baada ya kutiliana saini kitakachogharimu kiasi cha Bil 3.8 wilayani Sengerema mkoani Mwanza. Kivuko hicho kipya kitakuwa na uwezo wa kubeba uzito wa tani 50 ikijumuisha abiria 100 (waliokaa 50 na waliosimama 50) pamoja na magari madogo 6.*

# WATAALAM WA BARABARA LETENI MUAROBANI WA FOLENI MIJINI

Na **Shukuru Senkondo**




*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wadau wa Barabarabaada ya kufungua Mkutano wa Kimataifa wa Shirikisho la Barabara Duniani unaofanyika jijini Arusha.*

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa, amewataka watalaam wa barabara kutafuta suluhisho na mwarobaini wa changamoto zinazoikabilia miundombinu ya barabara mijini ikiwemo kupunguza msongamano wa magari na uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya miji.

Amesema hayo Jijini Arusha katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Arusha (AICC), wakati akifungua kongamano la Kimataifa la Shirikisho la Barabara Duniani (PIARC) litakalofanyika kwa siku tatu na kuhusisha wataalam wa hapa nchini, nchi za Afrika, Ulaya na Asia.

“Barabara ni mhimili mkubwa kwa nchi yetu kwani mizigo mingi inayotoka na inayoingia nchini kupitia Bandari husafirishwa barabarani “ ameeleza Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa ameeleza kuwa pamoja na kuboresha njia nyingine za usafiri kwa sasa Serikali inaendelea na uboreshaji wa reli ya kati na ujenzi wa reli ya kisasa kwa ajili ya kuipunguzia mzigo mkubwa barabara katika usafirishaji wa mizigo hasa inayokwenda mikoa ya mbali na bandari na nje ya nchi.

Aidha amewaagiza watalaam kukamilisha taarifa sahihi za kisayansi na kuwasilisha Wizarani wakati Serikali ikijiiandaa kufanya marekebisho ya Sera ya barabara hususani kwenye eneo la matumizi sahihi ya matairi mapana ‘Super Single’ hapa nchini ikiwa ni lengo la kuzilinda barabara nchini.

“Katika Mkutano huu mmejaa wabobezi kwenye mambo ya barabara ninachotegemea baada ya kikao hiki pamoja na mambo mengine mniletee utafiti uliofanywa kuhusu matumizi sahihi ya matairi mapana (super single tyre) ili tuweze kufanya maamuzi sahihi kwa Taifa letu” ameongeza Waziri Prof. Mbarawa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TARA, Bw, Joseph Haule ameeleza kuwa semina hiyo ya Kimataifa inayohusu masuala ya usafirishaji endelevu wa mizigo kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii imendaliwa na Shirikisho la Barabara Duniani (PIARC) kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) na Chama cha Wadau wa BarabaraTanzania (TARA) lengo likiwa ni kujadili na kutafuta ufumbuzi masuala mbalimbali ya barabara na hivyo kuleta tija.

# UJENZI NA UKARABATI WA VIVUKO KUTATUA CHANGAMOTO YA USAFIRI KANDA YA ZIWA

Na **Christina Seggu**



*Muonekano wa awali wa sehemu ya vivuko vinne vinavyojengwa na Kampuni ya Songoro Marine, mkoani Mwanza. Vivuko hivyo ni Kisorya – Rugezi (Ukerewe - Mwanza), Ijinga – Kahangala (Magu - Mwanza), Bwiro – Bukondo (Ukerewe - Mwanza) na Nyakalilo – Kome (Buchosa - Mwanza).*

Imeelezwa kuwa kukamilika kwa ujenzi wa vivuko vipya vinne na ukarabati wa vivuko vinne vitakavyotoa huduma katika maeneo mbalimbali ya Ziwa Victoria kutapunguza changamoto za usafiri kwa wananchi wanaoishi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kutarahisisha shughuli za maisha kwa urahisi, uhakika na usalama.

Hayo yamesemwa mkoani Mwanza na Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, wakati alipokagua karakana ya ujenzi wa meli na vivuko ya Songoro na kupata taarifa ya maendeleo ya ujenzi na ukarabati wa vivuko hivyo vitavyogharimu takribani bilioni 26 na kutarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti mwaka huu.

“Nimekagua na nimeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa vivuko vipya lakini pia na ukarabati wa vivuko unaoendelea, nimatumaini yangu vivuko hivi vitakamilika ndani ya muda kwani kuna baadhi ya maeneo vivuko hivyo havipo au kimebakia kimoja na hivyo kutokidhi mahitaji ya wananchi”, amesema Kasekenya.

Amefafanua kuwa kwa sasa ujenzi wa vivuko hivyo unaendelea na vipo katika hatua mbalimbali na kutaja kuwa vivuko hivyo ni Kisorya – Rugezi (Ukerewe - Mwanza), Ijinga – Kahangala (Magu - Mwanza), Bwiro – Bukondo (Ukerewe - Mwanza) na Nyakalilo – Kome (Buchosa - Mwanza).

Aidha, ukarabati wa vivuko unaoendelea ni pamoja na MV Misungwi (Kigongo - Busisi), MV Mara (Iramba - Majita), MV Ujenzi (Kisorya - Rugezi) na MV Nyerere (Bugolora - Ukara).

Aidha, ameiagiza Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), kumsimamia mkandarasi wa Kampuni ya Songoro kufunga vifaa vyote vilivyosanifiwa kuanzia katika hatua za awali hadi vivuko hivyo vitapokamilika.

Naye, Kaimu Meneja Vivuko Kanda ya Ziwa na Magharibi kutoka TEMESA Eng. Aloyce Ndunguru, amesema kuwa wanaendelea na ujenzi wa vituo vipya vitatu ambvyo ni Bwiro (kisiwani) – Bukondo katika Wilaya ya Ukerewe, Kituo ch Ijinga (kisiwani) – Kahangala katika Wilaya ya Magu na Kituo cha Mayenzi – Kanyinya ambapo miradi hiyo ikikamilika itafanya wawe na jumla ya vituo 16 katika kanda hiyo.

Ameeleza pia kanda hiyo ina jumla ya vivuko 17 ambapo kati ya hivyo vivuko vinne vipo katika matengenezo makubwa ambavyo ni MV Misungwi (Kigongo - Busisi), MV Mara (Iramba - Majita), MV Ujenzi (Kisorya - Rugezi) na MV Nyerere (Bugolora - Ukara).

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni ya Songoro Marine, Major Songoro, amemueleza Naibu Waziri huyo kuwa baadhi ya vivuko ambavyo vinafanyiwa ukarabati vipo katika hatua za mwisho za kukalimika na vitarudishwa TEMESA mapema kwa ajili ya kuendelea kutoa huduma.

# MIGIRE AAGIZA TPA KUANZA KUTOA HUDUMA BANDARI YA KWALA

Na **Biseko Ibrahim**



*Muonekano wa Bandari kavu ya Kwala.*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi anayesimamia Sekta ya Uchukuzi Bw.Gabriel Migire, amewaagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ( TPA) kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali na Binafsi kuhakikisha Bandari kavu ya Kwala inaanza kazi.

Migire ameyasema hayo kwenye Mkutano wa Maboresho ya Bandari ya Dar es salaam ambao umewakutanisha Uongozi wa Usimamizi wa Bandari (TPA), Wizara na wadau mbalimbali wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam.

“Bandari Kavu ya Kwala inatakiwa kuanza kazi haraka ili kupunguza msongamano wa shehena na Magari makubwa katika Bandari ya Dar es Salaama” alisema Migire.

Aidha, Migire aliongeza kuwa kukamilika kwa Bandari kavu ya Kwala kutasiadia kupunguza foleni ya magari makubwa katika jiji la Dar es Salaam, hivyo aliitaka kila taasisi ifanye wajibu wake ili bandari hiyo ianze kufanya kazi.

Kwa upande wake Meneja wa Bandari Kavu ya Kwala, Alexander Ndibalema, amesema kuwa ujenzi wa Bandari hiyo umefikia asilimia 90 na unatarajia kukamilika mwishoni mwa Mwezi Machi 2023, pia ujenzi wa Barabara ya Zege ya zaidi ya kilometa kumi na tano kutoka Vigwaza mpaka Bandari kavu ya Kwala imekamika.

Halikadhalika Ndibalema alifafanua kuwa Mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam itasafirishwa kwa treni mpaka Kwala hivyo anatarajia mizigo kwenda nje ya Tanzania na ndani ya Tanzania yote itachukuliwa katika Bandari hiyo.

Katika hatua nyingine Meneja wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Mrisho, amesema kuwa kwa sasa katika bandari ya Dar es Salaam Shehena imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 22 hivyo kutoa wito kwa kila mdau kuhakikisha anawahi kuhamisha mizigo hasa mizigo ya taasisi za Serikali ambayo inakaa baharini hapo kwa Muda mrefu.

# ERB NA EBK KUENDELEZA USHIRIKIANO TAALUMA YA UHANDISI

Na **Siti Said**




*Msajili wa Bodi ya Wahandisi (ERB), Mhandisi Bernad Kavishe, akizungumza na Waandishi wa Habari (hawapo pichani) mara baada ya kumalizika kwa kikao kazi kati ya Bodi ya Wahandisi wa Kenya na Tanzania, Jijini Dodoma.*

Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania (ERB) iameahidi kuendeleza ushirikiano na Bodi ya Usajili wa Wahandisi ya Kenya (EBK), katika mkataba wa makubaliano ya pamoja waliyoweka ili kuhakikisha wanakidhi vigezo vya ushindani katika nchi za umoja wa Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa kufunga warsha ya wiki moja iliyoandaliwa na ERB, jijini Dodoma, Msajili wa Bodi hiyo, Eng. Benard Kavishe, amesema kuwa dhumuni la warsha hiyo ni kuboresha mazingira katika taaluma hiyo ambapo itasaidia mhandisi kutoka Tanzania, Kenya pamoja na wale walio katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutambulika na kufanya kazi katika nchi hizo bila ya vizuizi vyovyote.

"Haya ni makubaliano ambayo tuliafikiana tangu mwaka 2012, lengo likiwa ni kuwasaidia wahandisi waliosajiliwa katika nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kufanya shuguli zao bila vizuizi na pia kukutana na kubadilishana uzoefu wa kitaalamu ili wote kuwa na viwango vinavyofanana", amesema Eng. Kavishe.

Aidha, Eng. Kavishe amefafanua kuwa tangu makubaliano hayo kuafikiwa kumekuwa na ziara na warsha za mara kwa mara kwa wahandisi hao ambapo kwa mwaka huu warsha ya kujengea uwezo wataalamu hao imefanyika jijini Dodoma.

Ametaja baadhi ya vigezo vilivyomo katika makubaliano yao ikiwa ni pamoja na kuwa na viwango sawa katika ufundishaji,usajili na kuwalea hali itakayorahisisha utendaji kazi na kufungua ajira katika nchi za Afrika Mashariki.

"Tulipokea ugeni wa watu Tisa kutoka Kenya ambao wamekuja kujifunza na kubadilishana uzoefu kati yetu ambapo tulichukuwa kutoka kwao kile ambacho hatuna na kile ambacho hawana wamechukua kwetu", amesema Eng. Kavishe.

Ameongeza kuwa baada ya ziara hiyo kumalizika anaamini kuwa wahandisi wa Tanzania na Kenya watafanana katika viwango vyao vya kiutendaji na hivyo kuendeleza ushirikiano na kuwa na ushindani dunia nzima.





*Baadhi ya Wajumbe wakimsikiliza Msajili wa Bodi ya Wahandisi Nchini (ERB), Mhandisi Bernad Kavishe, (hayupo pichani) wakati akifunga Warsha kati ya Bodi hiyo na Bodi ya Wahandisi kutoka Kenya (EBK), jijini Dodoma.*

Kwa upande wake, Mhandisi wa Bodi ya Usajili ya Kenya (EBK), Margaret Ogai, amesema kuwa kupitia warsha hiyo wamejifunza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja kuwa na utaratibu wa kufanya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaotoka vyuoni ambao wamesoma taaluma ya kihandisi, kuanzisha mfuko maalumu kwa ajili ya kusaidia wahandisi katika kuwapeleka mafunzo ya kuwajengea uwezo na kusajili wahandisi wengi wakike chini ya miaka 35.

Naye, Mhandisi kutoka Kenya ambaye ni mmoja wa washiriki wa warsha hiyo, Monica Wangari, amesema kuwa warsha hiyo imesaidia kujua masuala mengi ambayo anaamini kwa namna moja ama nyingine yataenda kufungua fursa ya ajira kwa wahandisi wengi wa Tanzania na Kenya pamoja na wale walio katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Amepongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maendeleo yaliyofanyika katika jiji la Dodoma ambapo licha ya mafunzo waliopata katika warsha hiyo pia walipata fursa ya kutembelea Mji wa Serikali, eneo la Mtumba, Dodoma na kuona namna ulivyopangika na kuvutia.

Mhandisi Veronica Ninalo kutoka ERB, ambae ni Mshiriki kutoka Tanzania uandaamesisitiza kwa Serikali kupitia Bodi hiyo kuandaa warsha za mara kwa mara ili kubadilishana uzoefu kutoka sehemu mbalimbali ili kuimarisha na kuboresha taaluma hii.

Ziara hii ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano ya pamoja katika nchi wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuendeleza na kukuza taaluma ya uhandisi.

# UTENDAJI KATIKA BANDARI YA MTWARA WAONGEZEKA

Na **Jacob Kipara**




*Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ( Sekta ya Uchukuzi) Mhandisi Aron Kisaka, akifafanua jambo kwa kamati ya maboresho ya bandari, wakati kamati hiyo ilipokutana mkoani Mtwara kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo.*

Imeelezwa kuwa maboresho makubwa yaliyofanywa katika bandari ya Mtwara yameongeza tija na utendaji wa bandari kwani takwimu zinaonyesha kukua kwa tani zilizohudumiwa kutoka laki 5 mwaka 2021/22 hadi milioni moja kwa mwaka 2022/23 na meli zilizohudumiwa kutoka 166 kwa mwaka 2021/22 hadi 180 kwa mwaka 2022/23.

Akizungumza wakati akifungua mkutano wa kamati ya Maboresho ya huduma za bandari kwa bandari ya Mtwara mkoani Mtwara, Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi, ambaye amemuwakilisha Katibu Mkuu-Uchukuzi Mhandisi Aron Kisaka amesema Serikali imedhamiria kuongeza ufanisi wa bandari zote nchini kwa kushirikisha wadau katika hatua zote za uendeshaji ili kuhakikisha zinakuwa na ufanisi mkubwa.

"Serikali imedhamiria kuhakikisha pato linalokusanywa kupitia bandari linavuka asilimia 50 na utekelezaji wa hili ulianza kwa kufanya maboresho ya miundombinu na sasa inakwenda na mkakati wa kushirikisha wadau ili kuja na suluhu ya pamoja kwa changamoto zinazojitokeza amesema Mhandisi Kisaka.

Mhandisi Kisaka ameitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kuhakikisha inaongeza juhudi kwenye masoko ili kuruhusu mashirika mengi zaidi kutumia bandari ya Mtwara hususani wakati huu ambao kuna mzigo mkubwa wa makaa ya mawe.

Aidha, Mhandisi Kisaka amesema Serikali inaendeleza juhudi za kuhakikisha inawakutanisha wadau wa ndani na wa nje hadi kufika mwezi Juni Wadau wa Tanzania na Zambia watakutana Tunduma lengo likiwa kujadili na kutafuta muarobaini wa changamoto za usafirishaji katika ukanda wa kusini mwa Tanzania.




*Baadhi ya wadau wa kamati ya maboresho ya bandari ya Mtwara, wakipitia makabrasha wakati wa kikao chao na Serikali mkoani Mtwara.*



*Muonekano wa Bandari ya Mtwara*

Kwa upande wake Meneja wa bandari ya Mtwara Norbert Kalembwe, amesema kupungua kwa tozo kwa bidhaa mbalimbali zinazosafirishwa kupitia bandari hiyo kumechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa mizigo.

Meneja Kalembwe ametumia fursa hiyo kuwataka wadau kujipanga kwa ajili ya msimu wa korosho kwani amewahakikishia kuwa makontena yapo na maeneo ya kuhifadhia mzigo yameshatengwa.

Serikali kupitia TPA imekuwa ikikutana na wadau wa bandari mara moja kwa mwezi lengo likiwa kuhakikisha changamoto zinazojitokeza zinajadiliwa na kupatiwa ufumbuzi kwa wakati na kwa kushirikisha wadau wote ili kuongeza ufanisi wa bandari hizo.

# BARABARA YA NORANGA HADI ITIGI KM 25 KUKUZA UCHUMI

Na **Neema Macha**



*Muonekano wa sehemu ya barabara ya Noranga - Itigi (km 25), inayojengwa kwa kiwango cha lami, mkoani Singida. Ujenzi wa barabara hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2024 kwa gharama ya shilingi Bilioni 29.770.*

Serikali imeanza kuunganisha mikoa ya nyanda za juu kusini kwa kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Makongorosi -Rungwa-Itigi hadi mkiwa sehemu ya Noranga hadi Itigi katika kitongoji cha Mlongojii chenye urefu wa kilometa 25 kwa upande wa mkoa wa Singida kwa lengo la kukuza uchumi wa mikoa hiyo.

Hayo yamesemwa wilayani Manyoni, mkoani Singida na Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, wakati alipokagua hatua ya ujenzi wa mradi huo pamoja na ujenzi wa barabara za mji wa Itigi (km 10) kwa kiwango cha lami.

Kasekenya ameeleza kuwa barabara hiyo ilikuwa ikitumika miaka ya 1970 kabla ya barabara ya TANZAM haijajengwa kwa kiwango cha lami na sasa Serikali imeona umuhimu wa kuijenga barabara hiyo na imetoa fedha kiasi cha shilingi Bilioni 29.770 kwa mkandarasi China Henan International Cooperation ya China ili kuikamilisha kwa muda wa miezi 18.

“Abiria waliokuwa wakisafiri kwenda Mbeya, Iringa na mikoa mingine ya nyanda za juu kusini kutoka kanda ya ziwa walikuwa wakija na treni mpaka itigi na kuchukuliwa na mabasi kwenda Mbeya na mikoa mingine ya nyanda za juu kusini hivyo barabara hii ni muhimu sana kiuchumi”, amefafanua Kasekenya.

Kasekenya ametoa maelekezo kwa Wahandisi Washauri kutoka Kitengo cha Usimamizi wa Miradi cha Wakala ya Barabara nchini (TANROADS) - TECU, kuhakikisha wanawasimamia wakandarasi hao kwa viwango vinachotakiwa na usanifu uliowekwa katika miradi hiyo.

“TECU dhamana mliyopewa ni kubwa katika usimimazi wa hii miradi na Rais wetu anatoa fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu anachokihitaji kutoka kwetu ni thamani ya fedha ionekane katika miradi ya barabara




*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala ya Barabara (TANROADS) mkoa wa Singida, Eng. Msama Msama, (mwenye suti) wakati alipokagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Noranga – Itigi (km 25) kwa kiwango cha lami, mkoani Singida.*

nchini", amesisitiza Naibu Waziri Kasekenya.

Aidha, Kasekenya amewaagiza TANROADS kushirikisha taasisi nyingine kama wana mipango miji, Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) pindi wanapofanya usanifu wa barabara hasa za mijini ili kuweza kuimarishwa kwa mifumo ya mifereji kwaajili ya maji kwani mvua zinaponyesha maji yanashindwa kwenda kwenye maeneo husika na kuleta kero hasa wanaopitiwa na barabara za mijini.

Pia ametoa wito kwa wananchi kuzitunza barabara hizo kwa kutokuzitumia vibaya ambapo amewasihi kuacha kupitisha mifugo, kumwaga mafuta, kuiba alama za barabara na madaraja na kutupa taka ovyo katika mifereji ya barabara hasa za mijini.

Pamoja na hayo Naibu Waziri Kasekenya ameridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo ambapo ikikamilika italeta mabadiliko makubwa sana ya kiuchumi, kimaendeleo na kijamiii kwa wananchi wa Itigi na Singida kwa ujumla.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Kemilembe Rose Lwota amemuahidi Naibu Waziri huyo kusimamia utekelezaji wa maagizo yote yaliyotolewa ikiwemo uwepo wa mifereji ya maji ili kuzuia maji ya mvua kuathiri baadhi ya makazi ya watu.

Naye Meneja wa TANROADS mkoa wa Singida, Eng. Msama Msama, ameeleza kuwa sehemu ya ujenzi wa Noranga hadi Itigi (km 25) mkandarasi ameshaleta mitambo yote kwa asilimia 75 na ameshaanza kazi ya kuzalisha kokoto za ujenzi ambapo kwa ujumla mradi umefikia asilimia 18 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Machi, 2024.

Ameeleza kuwa kwa upande wa mradi wa barabara za mji wa Itigi (km 10) unajengwa na mkandarasi mzawa kutoka kampuni ya Rocktronic kwa gharama ya shilingi Bilioni 8.598 kwa muda wa miezi 18 ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022 na mpaka sasa mradi umefikia asilimia 68.

# KM 612.14 ZA BARABARA KUJENGWA MKOANI MOROGORO

Na **Shukuru Senkondo**



*Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Morogoro Eng. Lazeck Alinanuswe, akieleza kwa vyombo vya habari utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya miundombinu ya barabara na madaraja mkoani humo.*

Imeelezwa kuwa kuanza kutekelezwa kwa ujenzi wa barabara mpya zenye urefu wa kilometa 612.14 kwa kiwango cha lami mkoani Morogoro kutaufungua mkoa huo kwa kuunganisha halmashauri zake zote kwa lami.

Hayo yamesema na Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Morogoro Eng. Lazeck Alinanuswe, wakati akieleza miradi ya kimkakati inayoendelea na ile inayotarajiwa kuanza kutekelezwa ambapo amefafanua kuwa miradi hiyo mipya zabuni zake zimetangazwa na iko katika hatua za mwisho ili kuweza kusainiwa ili kuanza utekelezaji.

Ameitaja miradi hiyo ikiwemo ujenzi wa barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere (Km 11.6), barabara ya Ifakara - Mbingu (km 62.5), barabara ya Mbingu - Chita JKT (km 37.5), barabara ya Ifakara - Lupiro - Mahenge/ Lupiro - Malinyi- Kilosa kwa Mpepo- Londo - Lumecha na Malinyi JCT - Malinyi (km 422.54) na barabara ya Bigwa - Mvuha (km 78) pamoja na madaraja ya Ruvu na Mvuha.

“Barabara hizi zote zikikamilika zitainua uchumi wa wananchi wa mkoa wa Morogoro pamoja na kuchochea maendeleo yake maana ni barabara za kimkakati”, amefafanua Eng. Lazeck.

Ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha za ujenzi wa miundombinu hiyo kwa mkoa huo ambayo inatarajiwa kuanza mapema iwezekanavyo.

Vilevile Eng. Lazeck ameeleza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Kidatu hadi Ifakara (km 66.9) kwa kiwango cha lami ambao umefikia asilimia 78 na unagharimu kiasi cha Bil 105.

"Ujenzi wa Barabara ya Kidatu hadi Ifakara unakwenda vizuri na hadi sasa mkandarasi amekamilisha km 43 za lami na kazi nyingine zinaendelea kwa hatua nzuri na kwa upande wa madaraja yote yamekwishakamilika kwa asilimia 83 na Daraja la Ruaha Mkuu imebakia kuweka kitako cha juu ili kazi likamilike", ameeleza Eng. Lazeck.

Amefafanua ujenzi wa barabara na daraja hilo unatekelezwa na mkandarasi Reynolds Construction Company kutoka Nigeria na kusimamiwa na kitengo cha usimamizi wa miradi cha TANROADS (TECU) unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Oktoba, 2023.

Aidha, ameeleza kuwa Serikali imetoa fedha kiasi cha Bil. 1.9 kwa ajili ya utekelezaji wa maboresho ya mizani ya Mikumi katika barabara ya Morogoro-Iringa (TANZAM Highway) na Mizani ya Michese katika barabara ya Dar es Salam-Morogoro kwa kuweka mizani ya kisasa inayopima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion) kwa lengo la kuzilinda barabara kwa kutoharibiwa na uzito mkubwa wa magari pamoja na kupunguza msongamano wa magari katika maeneo hayo.

Nao Wananchi wa Wilaya ya Ifakara wameishukuru Serikali kwani kukamilika kwa barabara ya Kidatu - Ifakara kumefungua fursa za kiuchumi Wilaya humo pamoja na mikoa ya jirani.



*Muonekano wa Sehemu ya barabara ya Kidatu – Ifakara (km 66.9), inayojengwa kwa kiwango cha lami mkoani Morogoro. Ujenzi wa barabara hiyo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu.*



*Muonekano wa Daraja la Ruaha Mkuu ambalo ni sehemu ya barabara ya Kidatu hadi Ifakara (km 66.9) inayojengwa kwa kiwango cha lami mkoani Morogoro ambao ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 78 na unagharimu kiasi cha Bil 105.*

# UKAGUZI WA KIWANJA CHA NDEGE CHA KIMATAIFA CHA MSALATO

Na **Mwandishi Wetu -** WUU






*Kazi ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Msalato zikiendelea, Jijini Dodoma ikiendelea.*





*Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, (Sekta ya Ujenzi), Balozi Aisha Amour akitoa na kupokea maelekezo kwa Mshauri elekezi wa Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, Mhandisi Shegan Berharie, wakati Katibu Mkuu huyo alipokuwa akikagua maendeleo ya mradi huo, jijini Dodoma.*

# WAZIRI PROF. MBARAWA AWAPONGEZA SCANIA KWA KUTIMIZA MIAKA 50

Na **Biseko Ibrahim**




*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akizungumza na wadau wa magari aina ya Scania wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya kampuni hiyo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akipiga honi kutoka kwenye gari la scania mara baada hotuba yake wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya kampuni hiyo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam*

# MBARAWA AITAKA SEKTA YA UJENZI KUSIMAMIA KIKAMILIFU MIRADI INAYOTEKELEZWA

Na **Siti Said**



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (wa tatu kulia waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa baraza la wafanyakazi Sekta hiyo, mara baada ya kufungua baraza la Sekta ya Ujenzi, Jijini Dodoma.*

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amewataka watendaji wa Sekta ya ujenzi kuhakikisha wanafuatilia na kusimamia miradi ya ujenzi inayotekelezwa ili kukamilika kwa wakati na kuwa na tija kwa wananchi.

Ameyasema hayo jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi na kusisitiza kuwa ufuatiliaji huo utasababisha miradi inayotekelezwa kulingana na thamani ya fedha iweze kuleta matokeo chanya na kuweza kukamilika kwa wakati.
"Napenda kuwakumbusha wajumbe kuwa mnatakiwa kuendelea kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kusimamia utekelezaji wa Miradi mbalimbali katika sekta ya ujenzi ikiwemo Barabara, Madaraja na Vivuko." amesema Profesa Mbarawa.

Aidha,Waziri Mbarawa amewatahadharisha watumishi wa Sekta hiyo kujiepusha na matumizi mabaya ya madaraka pamoja na ubadhirifu wa mali za umma, hali ambayo italeta taswira mbaya kwa taasisi na Wizara kwa ujumla.
Pia, ametoa rai kwa wajumbe wa baraza hilo kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia weledi, maarifa, uadilifu na uzalendo wa hali ya juu, utakaosababisha kufanikisha maendeleo ya taasisi na Serikali kwa ujumla.

Waziri Mbarawa amefafanua kuwa katika hatua ya kuongeza ufanisi na utoaji wa huduma, Watumishi wanatakiwa wapewe maeneo mahsusi ya kufanyia kazi, hali itakayosaidia kupima utendaji wa watumishi, kuwakuza, kuwapa morari ya kazi na kuwawezesha kuwa wabunifu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye pia ni Katibu Mkuu Sekta ya Ujenzi, Balozi Mhandisi Aisha Amour, amemhakikishia Waziri Mbarawa, kuwa Sekta ya Ujenzi itaendelea kutekeleza majukumu yake katika kuchangia maendeleo ya Taifa na kuzingatia viwango vya ubora wa ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja, nyumba za Serikali na Vivuko pamoja na Ujenzi na Upanuzi wa Viwanja vya ndege.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amewataka watendaji wa Sekta ya ujenzi kuhakikisha wanafuatilia na kusimamia miradi ya ujenzi inayotekelezwa ili kukamilika kwa wakati na kuwa na tija kwa wananchi.

Ameyasema hayo jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi na kusisitiza kuwa ufuatiliaji huo utasababisha miradi inayotekelezwa kulingana na thamani ya fedha iweze kuleta matokeo chanya na kuweza kukamilika kwa wakati.
“Napenda kuwakumbusha wajumbe kuwa mnatakiwa kuendelea kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kusimamia utekelezaji wa Miradi mbalimbali






*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akiteta jambo na Makamu wa Rais wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Bw. Thomas Ostros pembezoni mwa mkutano wa Biashara kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU) katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julias Nyerere jijini Dar es Salaam leo.*

# MENEJIMENTI YA SEKTA YA UJENZI YAKAGUA USIMAMIZI WA MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA MKOA WA TANGA NA PWANI

Na **Deniza Cyprian**





**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**
**Mji wa Serikali Mtumba**
**S.L.P 2888 Ujenzi**
**S.L.P 638 Uchukuzi**

**DODOMA**

**Simu: +255 26 23244455 / +255 26 2322703, 2322702**
**Nukushi: +255 26 2323233 / +255 26 2322704**
**Barua pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwt.go.tz**

wizarayaujenzinauchukuzi
wizaraUJnaUC
www.mwt.go.tz

#KAZIIENDELEE